JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU DESEMBA 2005 HADI DESEMBA 2008

1.0 UTANGULIZI

Dira ya Wizara ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.

Majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia Sera ya Afya na Ustawi wa Jamii na kutoa huduma za kinga na tiba, kudhibiti kemikali na kuendesha uchunguzi wa kisayansi wa magonjwa na sababu za vifo, kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vipodozi na chakula, kusimamia, kudhibiti na kuendeleza huduma za Tiba ya Asili na mbadala,kusimamia huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, kufanya ukaguzi wa huduma za afya zitolewazo katika ngazi mbalimbali, kuandaa, kusimamia, kuboresha utendaji na kuongeza upatikanaji wa wataalamu wa afya na ustawi wa jamii wenye utaalamu mseto unaohitajika katika ngazi mbalimbali, kuinua kiwango cha ushirikiano kati ya Wizara, Sekta Binafsi, Idara mbalimbali, Mashirika ya Umma na ya kimataifa na Asasi mbalimbali katika Sekta ya Afya ili kuongeza na kuimarisha ubora wa huduma za afya, kuongoza na kusimamia wakala za Serikali zilizo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuongoza na kusimamia taasisi na mashirika ya umma na miradi iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii,kushiriki katika juhudi za kimataifa za kuimarisha huduma za afya kwa kuwa wanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa zinazojishugulisha na huduma za afya,kuratibu, kutekeleza na kusimamia masuala ya lishe nchini, kufanya utafiti wa magonjwa ya binadamu na kutumia

matokeo kwa manufaa ya wananchi, kulinda haki za makundi maalum ambayo ni watu wenye ulemavu, watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi, wazee wasiojiweza na watoto walio katika mkinzano wa sheria na kusimamia na kutoa huduma za dharura wakati wa maafa pamoja na kujiandaa kwa majanga.

Huduma za afya nchini zinatolewa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanyika katika sekta ya afya kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma bora za afya mjini na vijijini.

Katika kipindi cha Miaka mitatu kilichoanza Desemba 2005 hadi Desemba 2008, huduma zimetolewa kwa kuzingatia Sera, Dira, Dhamira na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile MKUKUTA, Mkakati wa Kitaifa 2025, malengo ya maendeleo ya millennia, pia kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010.

Waziri imetengeneza mazingira mazuri ya kuiwezesha sekta ya afya kutimiza wajibu wake kitaifa na kwa wananchi kwa mafanikio makubwa.

Juhudi mbalimbali zilizofanyika katika ngazi ya kimataifa, kitaifa na kwa wananchi ni kama ifuatavyo:

- Mheshimiwa Waziri alihudhuria mkutano wa kimataifa wa malaria nchini Marekani ambapo alikutana na Bill Gates na Mkewe Mellinda Gates kukubali kusadia Tanzania katika mpango wa udhibiti wa malaria. Aidha, asasi ya kimataifa ya MACEPHA kusaidia Afrika ikiwemo Tanzania katika ufuatiliaji wa udhibiti wa malaria.

- Mh. Waziri alihudhuria mkutano maalum Umoja wa Mataifa uliotambua mafanikio makubwa kutokana na juhudi za uongozi wa juu wa serikali akiwemo Mh. Rais katika suala la upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI nchini, ambapo watu zaidi ya milioni nne walipimwa.

- Mh. Waziri alifanikiwa kushawishi wajumbe wa mkutano wa SADC mjini Durban Afrika Kusini, kuwa na sauti moja katika mpango wa udhibiti wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Neglected Tropical Diseases) kama vile Usubi (Onchocerciacis), Vikope (Trachoma), Matende na Ngirimaji kwa ajili ya kuongeza raslimali zaidi za kudhibiti magonjwa haya.

- Wizara imefanikiwa kupata nafasi 20 za masomo ya udaktari kwa gharama za Serikali ya Cuba Aidha, Cuba wamekubali kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa madaktari nchini kwa kuwaleta madaktari wa Cuba kuja kufanya kazi nchini.

    - Wizara imefanikiwa kuishawishi Serikali ya Italy kugharamia huduma za tiba ya saratani katika Hospitali ya Rufaa Bugando kwa ajili ya kutoa huduma katika kanda ya Ziwa na ya Magharibi.

- Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu udhibiti wa ugonjwa wa matende na ngirimaji (Global Alliance on Elimination of Lymphatic Filariasis) ambapo mheshimiwa Rais alizindua mfuko maalum.

- Kitaifa pia amehudhuria vikao vya baraza la mawaziri ambapo nyaraka mbalimbali zinazohusu uundwaji wa sheria katika sekta ya afya zilipitishwa. Pia mheshimiwa Waziri na Naibu wake wameendelea kuhudhuria vikao vya bunge pamoja na kujibu maswali mbalimbali yanayohusu sekta ya afya na ustawi wa jamii.

- Kushiriki kwenye ziara za Mheshimiwa Rais mkoani Tanga na Mbeya na kamati ya Bunge ya huduma za jamii, mkoani Manyara, Morogoro, Iringa na Dodoma ambapo walikutana na wananchi.

- Kufanya ziara za kikazi za kukagua na kuona shughuli za utoaji wa huduma za afya katika hospitali za mikoa , wilaya, vituo vya afya na zahanati katika mikoa ya Tabora, Ruvuma, Tanga na Singida.

- Kufanya mikutano ya hadhara na ya ndani kusikiliza kero za wananchi pamoja na watumishi wa sekta ya afya na ustawi wa jamii.

Pia Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia kanuni na taratibu zote za utoaji wa huduma za sekta ya afya na ustawi wa jamii nchini, ambapo wafanyakazi wameendelea kutoa huduma kwa juhudi kubwa na mafanikio ya juu. Aidha, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:

    - Vikao vya makatibu wakuu ambapo masuala ya sekta nyingine zenye uhusiano na sekta ya afya na ustawi wa jamii na kuwezesha sekta ya afya kuendelea kupata kipaumbele katika bajeti na kuwa ya tatu.

    - Vikao vya majadiliano na wadau wa maendeleo wa sekta ya afya pamoja na kushiriki vikao vya aina hiyo katika ngazi ya kitaifa ambapo sekta ya afya imeendelea kuungwa mkono na kuendelea kupata misaada.

    - Ziara za kutembelea watendaji katika mikoa ya, Morogoro, Mwanza, Arusha, Mara, Tabora, Dar es Salaam na Tanga na pia katika ziara za Mheshimiwa Rais katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga na Dodoma.

- Vikao vya bodi ya ushauri ya ECSA health ambapo Tanzania ni Mwenyekiti, Visiwa vya Shelisheli na Arusha Tanzania, ambapo masuala mbalimbali ya afya kikanda yalijadiliwa.

2.0 MAFANIKIO MENGINE

Wizara kama kiungo muhimu katika kutekeleza shughuli zake za utawala, uendeshaji na utumishi, ni kama yafuatayo:

2.1.1 Kuwapangia vituo Watumishi wa Kada za Afya.

- Katika kipindi cha Desemba, 2005 hadi Desemba 2008 jumla ya watumishi 10,814 wa kada mbalimbali za Afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Mafundi sanifu, Wazoeza Viungo, Maafisa Wauguzi, Wafamasia, Wahudumu wa Afya, Tabibu na Makatibu wa Afya wamepangiwa kufanyakazi katika Sekretarieti za Mikoa yote, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji, na Wilaya zote na katika baadhi ya Wizara. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 63 ya vibali vyenye wataalamu 17,245 vilivyotolewa katika kipindi hicho. Idadi hiyo ya kuwapangia wahitimu wa kada za afya imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonyesha hapo chini:

MWAKA	KIBALI	WATAALAMU	ASILIMIA
2005/2006	1,677	983	58.17
2006/2007	3,890	3,669	94.31
2007/2008	6,437	4,812	74.75
2008/2009	5,241	1,350*	25.75*

*Zoezi la kuwapangia vituo vya kazi linaendelea.

- Kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya kiserikali ya Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, wataalamu wa afya 275 wameajiriwa na wapo katika Halmashauri 52 nchini.

2.1.2 Mishahara

- Aidha, katika kipindi cha 2006-2008, Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Afya imeboreshwa. Kwa sasa watumishi wa kada za afya ndiyo wanaolipwa mishahara mikubwa zaidi ikilinganishwa na watumishi wa kada nyingine

katika utumishi wa umma. Hali hii imewavutia watu wengi waliosomea fani mbalimbali za Afya kuingia kwenye Utumishi wa Umma.

2.1.3 Upandishwaji vyeo

- Katika kipindi cha 2006-2008 wizara imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 2,061 ambao wapo chini ya mamlaka ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

2.1.4 Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada za Afya.

- Wizara imefanya marekebisho ya Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada za Afya ili kujumuisha baadhi ya kada ambazo awali hazikuwa kwenye muundo huo kama vile Maafisa Wuguzi, Maafisa Afya na Wazoeza Viungo ngazi ya Shahada, kutenganisha sifa za Madaktari wa Kawaida na Madaktari Bingwa, kujumuisha kada mpya za matabibu wasaidizi, wasaidizi wa maabara, maafisa afya wasaidizi n.k. zilizoanzishwa ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya Msingi (MMAM) ambao unalenga kuwa na zahanati katika kila kijiji na vituo vya afya kwa kila kata. Aidha, katika Muundo huo umeongezwa kada ya Maafisa Lishe ambayo imeanzishwa ili kukabiliana na tatizo la lishe nchini ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na magonjwa ya moyo.

2.1.5 Muundo wa Wizara (Organization Structure)

Kufuatia mabadiliko ya Wizara yaliyaofanywa mwaka 2006 kwa kuiunganisha Wizara ya Afya na Idara ya Ustawi wa Jamii; Wizara ililazimika kubadili Muundo wake ili kuendana na mabadiliko husika. Hivi sasa Muundo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Organization Structure) tayari umekamilika na kupitishwa.

2.1.6 Taratibu za uendeshaji wa huduma za afya

- Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Wizara imeandaa taratibu za Uendeshaji wa huduma za afya nchini. Taratibu hizi zimeundwa ili kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

2.1.7 Ofisi ya Malalamiko

- Wizara imeanzisha Ofisi ya Maalum ya kushughulikia malalamiko yanayohusiana na mwenendo mzima wa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa malalamiko yanafanyiwa kazi pale yanapotokea. Tangu ofisi ilipofunguliwa Julai, 2007 mpaka sasa Wizara

imepokea jumla ya malalamiko 117. Aidha, jumla ya malamiko 92 tayari yamefanyiwa kazi kwa kupatiwa ufumbuzi.

2.1.8 Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Sekta ya Afya

- Mwaka 2008, Wizara imeunda Baraza la Majadiliano ya pamoja la Sekta ya Afya (Joint Negotiation Committee). Madhumuni ya kuundwa kwa Baraza hili ni kuimarisha ufuatiliaji wa maslahi ya watumishi wa afya.

2.1.9 Huduma za Usafirishaji

- Wizara imetoa mwongozo wa kuendesha, kusimamia na kudhibiti mfumo wa usafirishaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini. Matumizi ya mfumo katika kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake yameleta mafanikia yafuatayo:

  - Kupunguza viwango vya matumizi ya mafuta kwa kuhakikisha kuwa magari yanatumia mafuta kulingana na viwango vilivyowekwa na watengenezaji (Km 6-8 kwa lita moja ya mafuta)

  - Kupunguza gharama za matengenezo na kuongeza uhai wa magari katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya kwa wastani wa miaka mitano ikilinganishwa na awali

2.2 SERA NA MIPANGO

Idara ya Sera na Mipango ni kiungo muhimu katika kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu Sera ya Afya, Uandaaji wa Mipango, Bajeti na uratibu wa shughuli zote za ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini, masuala ya kisheria, Mabadiliko katika Sekta ya Afya, na uratibu wa matumizi ya mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Huduma za Afya (MTUHA).

Aidha masuala mengine ni pamoja na kuratibu mahusiano ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na EAC, SADC na AU, katika masuala ya kisera na rasilimali ikiwemo fedha na kuratibu kazi za wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya. Katika kipindi cha kuanzia Disemba 2005 hadi Disemba 2008, mafanikio yafuatayo yamepatikana:

2.2.1 Sera ya Afya

- Wizara imeandaa Sera mpya ya Afya kwa kupitia sera ya mwaka 1990. Sera hii imepitishwa mwaka 2007. Maboresho yamelenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora karibu na wananchi, ushirikishwaji wananchi katika kupanga, kubuni mbinu mpya na kuchangia huduma za afya**.**

Maeneo ya kipaumbele kwenye Sera hii ya Afya 2007 ni:

- Huduma za afya ya msingi
- Huduma za kinga ikiwemo huduma ya mama na mtoto
- Huduma za tiba zikiwemo huduma za uchunguzi wa magonjwa, dawa na tiba asili/ mbadala
- Mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na uwekaji usimamizi wa ubora wa viwango.
- Mfumo wa sheria

2.2.2 Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM)

- Wizara imeandaa mpango kabambe wa MMAM 2007-2017. Lengo la mpango huu ni kuongeza kasi ya utekelezaji wa kupeleka huduma kwa wananchi kwa kujenga Zahanati kila Kijiji, kituo cha afya kila Kata na hospitali ya Wilaya. Hii ni pamoja na kukarabati vyuo vya afya vilivyopo na kuongeza wanafunzi kwenye vyuo hivyo. Vituo hivi vitawezesha kutoa huduma zote zilizo katika sera.

2.2.3 Mpango mkakati wa afya wa awamu ya tatu

- Kuandaa na kupitisha mpango mkakati wa miaka sita 2009/15 wa kuongeza ufanisi na kasi katika utoaji wa huduma za afya. Wadau wote wamehusishwa wakiwemo washirika wa maendeleo. Mkakati unalenga ngazi zote za huduma kuanzia kaya, kata, wilaya, mkoa na taifa ili kuboresha upatikanaji wa rasilimali watu, fedha, vifaa na miundombinu.

2.2.4 Mabadiliko katika sekta ya afya

- Mabadiliko ya Sekta ya Afya yanaendeshwa kwa mfumo wa majadiliano ya pamoja ya kisekta (Sector Wide Approaches-SWAP)
- Serikali imeridhia utaratibu wa kutumia mpango huu pamoja na “Health Basket Fund” (HBF), na wengine kutumia miradi na Taasisi zisizo za Kiserikali -NGOs. Fedha hizo zote zinaingizwa kwenye MTEF.

2.2.5. **Ushiriki katika kupima Mafanikio ya Serikali (GBS-PAF)**

- Serikali imeridhia mpango huu wa Maendeleo ikishirikiana na wadau wa maendeleo na sekta ya afya imeweza kushiriki vikao vyote kwa mafanikio. Mafanikio hayo yamewahamasisha wadau wa maendeleo kuendelea kutoa michango yao kupitia GBS/PAF na Basket Fund

2.2.6 Serikali na wadau wa maendeleo

- Kwa kushirikiana na wadau wa mfuko wa maendeleo wa pamoja kumekuwa na ongezeko la fedha inayotengwa kutoka dola za Kimarekani 0.5 kwa mwaka 2006 hadi dola moja kwa kila Mtanzania mwaka 2008. Fedha hizi zimepelekwa kwenye Halmashauri ambako ndiko wananchi wengi wanakoishi.Maamuzi ya matumizi ya fedha hizi hufanywa na halmashauri zenyewe kwa ajili ya kuboresha huduma za afya chini ya mfumo wa ugatuaji wa madaraka"D by D".Mfumo huu umehamasisha wahisani kuingia basket funds kutoka watano (5) hadi kufikia 13.

2.2.7 Mchango wa wananchi (CHF, NHIF na Cost Sharing)

- Wananchi wameshiriki katika michango mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma nchini. Michango hii imepatikana kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na uchangiaji wa moja kwa moja (Cost Sharing).Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi waendelee kuchangia huduma za afya.

2.2.8 Mapitio ya sekta ya afya kwa pamoja na wahisani ya kila mwaka

- Sekta ya Afya imefanya mapitio kwa miaka tisa mfululizo. Mapitio haya yamesaidia kupima ufanisi wa Sekta kiutekelezaji. Wadau wamejenga imani kubwa na Serikali. Kwa sasa fedha zinazoto;ewa na mfuko wa Pamoja (Health Basket Fund) ni kiasi cha shilingi 96,145,100,040 kwa mwaka 2008/ 2009 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi 56,400,000,000 cha mwaka 2005/2006. Ongezeko hili ni sawa na asilimia ...

2.2.9 Tathmini ya sekta ya afya

- Tathimini ya miaka 6 kuanzia 1999 hadi 2006 ilifanyika mwaka 2007. Tathimini hii imebaini kwamba ubora wa huduma umeongezeka, vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimepungua kutoka 99 hadi 68 kati ya mwaka 2005 hadi 2008 kwa kila 1000 waliozaliwa hai. Upatikanaji wa fedha umeongezeka hasa kupitia Health Basket fund.

2.2.10 Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia

- Utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya milenia ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupunguza kasi ya kuambukiza kwa UKIMWI, Malaria, Kifua kikuu na kuhudumia waathirika umeendelea vizuri. Vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na miaka mitano vimepungua kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali: Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila watoto 1000 wanao zaliwa hai

Umri	**2005**	**2008**
Watoto wachanga chini ya siku 28	32	29
Watoto chini ya mwaka mmoja	68	58
Watoto chini ya Miaka 5	112	91

Angalizo: lengo la milenia ni kupunguza vifo hivi mpaka 54 ifikapo mwaka 2015

2.2.11 Huduma za Afya katika ngazi ya Halmashauri

- Katika kutekeleza mpango wa serikali wa kupeleka madaraka na rasilimali katika ngazi ya Halmashauri, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI, imefanya yafuatayo:
  - Kuandaa miongozo na mipango ya afya katika Halmashauri
  - Kuratibu na kutoa ushauri kuhusu Mipango Kabambe ya afya ya Halmashauri
  - kuandaa miongozo ya mipango ya vituo vya afya na zahanati
  - Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa kupunguza vifo vya mama na mtoto katika Halmashauri kwa kutoa motisha kwa wafanyakazi
  -

2.2.12 Takwimu

Mafanikio

- Utafiti kuhusu upatikanaji wa huduma za afya (Service Availability Mapping Survey) ulifanyika katika mikoa na halmashauri .Takwimu zilizopatikana zimesaidia katika kupanga Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uboreshaji wa sera ya afya na kupanga mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za afya. Utafiti huu umesaidia kujua ni sehemu zipi za nchi ambazo hazijafikiwa na huduma muhimu za kiafya kama vile vyandarua, dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, kifua kikuu, tiba ya malaria n.k

- Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Takwimu, kufanya tafiti zifuatazohzifuatazo:

  -Huduma zitolewazo pamoja na ubora wake (Tanzania Service Provision Assessment Survey 2006)

  - Hali ya ugonjwa wa UKIMWI na malaria. Aidha utafiti huu pia ulifanywa kwa ushirikiano na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)

    Tafiti hizi zimesaidia kutoa viashiria mbalimbali vya MKUKUTA, malengo ya Milenia na mwenendo wa huduma zinazotolewa katika sekta ya afya. Aidha tafiti hizi zimesaidia kujua mwenendo mzima wa janga la UKIMWI hapa nchini jambo ambalo limesaidia kujipanga upya katika kukabiliana na janga hili.

- Mafunzo ya utafiti kwa timu za uendeshaji wa Afya za wilaya na mikoa katika mikoa kumi (10) ya Tanzania bara yamefanyika, ambayo ni Mwanza, Kagera, Mara, Dodoma , Shinyanga, Ruvuma,Manyara,Mtwara, Lindi, na Kilimanjaro.

- Tovuti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeunganishwa na tovuti zingine za taasisi zinahusiana na kutoa huduma za afya hapa nchini (www.moh.go.tz) ili kuboresha mawasiliano na upatikanaji wa taarifa.

2.2.13 Sheria

Kitengo cha sheria katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kina jukumu la kupitia na kutoa ushauri kuhusu sheria mbalimbali zinazoandaliwa na Wizara pamoja na taasisi zake. Aidha, será ya afya ya 1990 ilifanyiwa mapitio na kupitishwa 2007 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Kutokana na mabadiliko hayo, sheria zifuatazo zimeweza kuandaliwa na kupitishwa:

- Sheria ya Usajili wa wataalam wa Maabara za Afya 2007

- Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mionzi na Radiolojia 2007
- Sheria ya wataalam wa Macho 2007
- Sheria ya kuzuia na kudhibiti Virusi vya Ukimwi (VVU) 2008
- Sheria ya Afya ya Akili 2008

Aidha kuna miswada ambayo Wizara iko katika hatua mbalimbali za maandalizi. Miswada hiyo ni pamoja na:

- Muswada wa Teknolojia ya DNA
- Muswada wa Afya ya Jamii

Marekebisho ya sheria ya Bima ya Taifa ya Afya yatafanyika kwa kupitia vipengele vya sheria hiyo ili kuwajumuisha wanachama wastaafu pamoja na madiwani.

2.3 OFISI YA MGANGA MKUU WA SERIKALI

Mganga Mkuu wa Serikali ni msimamizi mkuu wa sera na utekelezaji wa idara za kinga, tiba na mafunzo na maendeleo ya utumishi wa afya. Wajibu wake mkubwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Waziri na Katibu Mkuu kuhusu masuala yote yanayohusu taaluma ya afya. Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali pia inasimamia na kufuatilia vitengo vitatu na mabaraza ya kitaaluma matano. Mafanikio ya sehemu hizo ni kama ifuatavyo:

2.3.1 **Huduma za Uuguzi na Ukunga**

- Kutayarisha miongozo ya kiuuguzi na ukunga ili kuelekeza jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma za Uuguzi na Ukunga kwa kuzingatia viwango vya ubora. Miongozo hiyo ni pamoja na:
    - Basic Nursing and Midwifery Procedure Manual
    - Minimum Standards for Nursing and Midwifery Practice
    - Tanzania Nursing and Midwifery Model of Practice
    - Minimum equipment and supplies required for nursing and midwifery procedures
    - Nurses and Midwives Guidelines and Protocols for Preventing HIV/AIDS from needle stick and sharps injuries in Tanzania

- A Standard Checklist for monitoring and supervising nursing and midwifery services in the country

- Kufundisha na kufafanua (dissemination) kwa wahusika miongozo mbalimbali ya kisera iliyoorodheshwa hapo juu kwa lengo la kuiweka katika mipango ya mikoa na wilaya kwa ajili ya utekelezaji kwa lengo la kuinua ubora wa utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga.
- Mwongozo wa Maadili ya uuguzi na ukunga umetayarishwa na Baraza na kufanyiwa mafunzo kwa viongozi wa wauguzi ili kuendelea kuimarisha nidhamu na maadili ya taaluma sahihi.
- Tafiti za kujua hali ya utoaji na ubora wa huduma za afya na uuguzi zimefanyika na uendelezaji wake unaendelea. Matokeo ya tafiti hizi zitasaidia katika kufanya maamuzi sahihi na kuweka mikakati ya jinsi ya kuinua ubora wa huduma hizi.
- Mafunzo ya Uongozi (*Leadership for Change*) na utafiti yametolewa kwa wauguzi wakuu wa mikoa na wauguzi wakuu wa hospitali ili kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma katika mikoa na wilaya.
- Kitengo kimekuwa kikitayarisha na kuendesha vikao vya tathmini ya huduma za uuguzi nchini na wauguzi wakuu wa mikoa na hospitali za rufaa, hivyo kuboresha utoaji wa huduma za uuguzi.

2.3.2 Dharura na Maafa

Kitengo cha Maafa na Dharura ni moja ya vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali kikiwa na majukumu ya kushughulikia majanga na dharura mbalimbali katika sekta ya afya. Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Desemba 2005 hadi Desemba 2008, Kitengo kimeweza kupata mafanikio katika mambo yafuatayo:

- Kuanzisha Timu ya Dharura ya Kitaifa (National Rapid Response Team) yenye wataalam 40. Timu hiyo imegawanyika katika makundi mawili, ya dharura zinazohitaji huduma za kiupasuji ***(surgical cases)*** *na* dharura zinazohitaji huduma za tiba ***(medical cases)***.

- Kushiriki na kufanikisha udhibiti wa mlipuko wa ugonjwa wa Rift Valley Fever (RVF) katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Morogoro, Iringa na Manyara, mwishoni mwa mwaka 2006.

- Kushiriki katika juhudi za uokoaji na uhifadhi wa miili ya wachimbaji waliokufa kutokana na mafuriko ndani ya migodi ya Mererani, Simanjiro, mkoani Manyara Februari mwaka 2008.

- Kushiriki katika uchunguzi wa athari za kiafya zilizotokana na mlipuko wa moshi mzito katika Mlima wa Oldonyo Lengai mkoani Arusha mwanzoni mwa mwaka huu (2008), hali iliyohisiwa kuathiri afya za wakazi wa maeneo hayo, kutokana na viwango vya juu vya madini na kemikali ambavyo vina athari kwa binadamu.Taarifa hiyo imetumika kuhamasisha wananchi kuhamia katika sehemu salama.

- Kujenga uwezo wa mikoa katika kukabiliana na majanga na dharura mbalimbali kwenye maeneo yao kwa kutoa mafunzo maalum juu ya 'Mass Casualty Management' kwa Kamati za Uendeshaji Huduma za Afya Mkoani katika mikoa yote 21.

- Kujenga uwezo wa mikoa katika kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa Ebola na Marburg kwa kuendesha mafunzo ya dharura kwa watumishi wa afya katika mikoa ya Kagera, , Rukwa, Mbeya, Mwanza na Mara, baada ya kutokea ugonjwa huo katika nchi jirani za DRC na Uganda mwaka 2006/2007.

- Kugawa vifaa tiba vya dharura pamoja na dawa katika hospitali za Tumbi, Mkoa wa Pwani, na hospitali za mikoa ya Morogoro na Dodoma kufuatia matukio ya ajali za barabarani mwaka 2006 na 2007 yaliyosababisha vifo na majeruhi wengi kulazwa katika hospitali hizo.

2.3.3 Mabaraza ya kitaaluma

Mabaraza ya kitaaluma yanasimamia maadili ya taaluma mbalimbali za afya

2.3.3.1 Baraza la Macho na Miwani

- Sheria mpya "Optometry Act" 2007 imepitishwa na Bunge na kuelimisha wataalamu katika mikoa ya kanda za Mashariki na Kaskazini.

- Kuandaliwa na kuchapishwa kwa kitabu cha maadili na mwenendo wa utendaji kazi kitaaluma kwa wataalam wa upimaji macho na miwani.

- Kuandaa mtaala mama kwa wataalamu wa upimaji macho na miwani (Generic Curriculum).

2.3.3.2 Baraza la Wauguzi na Wakunga

- Kukamilika kwa zoezi la kuhakiki vyeti vya wauguzi wote 22,000 Tanzania kwa kushirikiana na wauguzi viongozi katika ngazi za mkoa na wilaya. Jumla ya vyeti 64 vilibainika kuwa ni vya kughushi na wahusika walichukuliwa hatua za kisheria.

- Leseni za Awali na za Marudio zilitolewa kwa Wauguzi 22,000 Tanzania (license for practice).
- Baraza limeanzisha mfumo wa taarifa za Wauguzi na Wakunga wote "*Data Bank*", ili kurahisisha kuwepo kwa kumbukumbu sahihi. Kwa sasa Baraza limekamilisha jumla ya kumbukumbu 22,000 za Wauguzi na Wakunga ambazo tayari zimeisha ingizwa kwenye mfumo huu. Zoezi hili limesaidia kuboresha kumbukumbu za Baraza, kuhakiki usajili wa Wauguzi na kurahisisha upatikanaji wa takwimu muhimu zinazohusiana na rasilimali watu.
- Tuhuma 14 dhidi ya Wauguzi waliovunja maadili zilisikilizwa na kutolewa hukumu. Katika tuhuma hizo, tuhuma 10 wauguzi walipatikana na hatia na adhabu mbalimbali zilitolewa ikiwa ni pamoja na kuonywa, karipio na kusimamishwa kwa muda.

- Baraza limeendesha mafunzo kwa Wauguzi Wafawidhi wa hospitali zote za Rufaa, Mikoa, Wilaya na kuwajengea uwezo katika kusimamia maadili na utendaji kazi pamoja na kurudisha taswira nzuri ya Uuguzi nchini.

- Miongozo mbalimbali inayohusiana na Taaluma ya uuguzi na Ukunga imeandaliwa nakufanyiwa rejea kama ifuatavyo:
    - Mwongozo wa kuendesha huduma binafsi za uuguzi
    - Mwongozo wa Maadili
    - Mwongozo wa utoaji taarifa kuhusu Muuguzi asiyezingatia maadili ya kazi na uuguzi pia.
    - Mwongozo wa mafunzo na viwango vya stadi za taaluma ya uuguzi
    - Mwongozo wa mafunzo na utoaji wa huduma zifuatazo:
        - Uuguzi na utoaji nusu kaputi
        - Uuguzi na huduma za Afya ya akili
        - Uuguzi na huduma ya macho
        - Stadi za kuokoa maisha kwa wazazi na watoto wanaozaliwa

- Kanuni za maadili ya Uuguzi
- Mwongozo wa kuwafundisha na kuwasimamia wanafunzi wauguzi katika sehemu za huduma

2.3.3.3 Baraza la Tiba Asili na Mbadala

Baraza limeweza kutayarisha kanuni na miongozo mbalimbali zifuatazo:

- Kanuni za usajili wa waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala pamoja na wasaidizi wao na vituo rasmi vya tiba asili na tiba mbadala.
- Kanuni zinazohusu maadili na utendaji wa taaluma ya tiba asili na tiba mbadala.
- Kanuni za kukusanya maduhuri (fees and charges) ya Baraza.
- Kanuni za kuendesha Baraza (inquiry procedures)
- Mwongozo wa Vituo vya kutolea huduma za tiba asili na tiba mbadala (Standard guidelines of traditional and alternative health facilities in Tanzania Mainland).
- Mwongozo wa Usimamizi na Ukaguzi wa huduma tiba asili na tiba mbadala (National supervision guidelines for quality traditional and alternative health care services)
- Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Baraza.
- Mwongozo wa Kufundishia Urasimishaji wa tiba asili na tiba mbadala.
- Maafisa Watendaji wa Kata katika mikoa ya Iringa na Pwani walielimishwa kuhusu sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala na jinsi Ofisi zao zinavyohusika na usajili wa Watoa huduma wa tiba asili.

2.3.3.4 Baraza la Famasi

Katika kipindi cha miaka mitatu 2005 – 2008 Baraza limeweza kupata mafanikio katika maeneo yafuatayo:

- Kuandaa na kukamilisha kanuni za Usajili wa wanataaluma (Regulations for Registration, Enrollment and Enlistment of Pharmacists, Pharmaceutical techinicians and Pharmaceutical assistants).

Baraza limefanikiwa kusajili wanataaluma kama inavyooneshwa hapa chini:-

MWAKA	IDADI YA WAFAMASIA (PHARMACISTS)	IDADI YA PHARM TECHS	IDADI YA PHARM ASSTS
2006	560	126	110
2007	674	386	331
2008	700	420	349

- Kuandaa Kanuni za Elimu na Mafunzo (Education and Training Regulations), ambazo zinatumika katika kusimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa stashahada ya Famasi
- Kuandaa mitaala ya mafunzo ya kujiendeleza kazini kwa taaluma ya famasi.
- Kanuni na Miongozo ifuatayo imeandaliwa:
  - Taratibu za kuendesha mahojiano kwa wanaotuhumiwa kukiuka maadili
  - Maadili na miiko ya wanataaluma
- Kuhamasisha/kuelimisha wanataaluma na wadau wa taaluma ya Famasi kwa njia ya:
  - Kuandaa vipeperushi na kusambazwa kwa walengwa
  - Kuandaa vitabu vya Sheria, Kanuni na Miongozo iliyokwisha pitishwa vinasambazwa kwa walengwa
- Ili kupunguza upungufu wa wanataaluma wafamisia, Wizara imeongeza vituo vya kufanyia Mafunzo ya vitendo (Internship centers) kutoka Vituo vine (4) hadi kufikia kumi (10) kwa sasa. Vituo vilivyoongezeka ni:
  - Hospitali ya mkoa Mtwara (Ligula hosp)
  - Hospitali ya mkoa Tanga (Bombo hosp)

- Hospitali ya mkoa Arusha (Mt. Meru hosp)
- Hospitali ya Manispaa Ilala (Amana hosp)
- Hospitali ya Manispaa Kinondoni (Mwananyamala hosp)
- Hospitali ya Manispaa Temeke (Temeke hosp)

2.3.3.5 Baraza la Madaktari Tanganyika

- Hadi sasa Baraza limefanikiwa kutengeneza " Codes of Ethics" ambayo ni mwongozo wa maadili ya wanataaluma.
- Baraza limetengeneza mfumo wa takwimu (Data Base) kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za wanataaluma waliosajiliwa na Baraza.
- Baraza limeingiza majina ya madaktari wote nchini katika kompyuta mfumo wa "Spreadsheet" ili yaweze kuharirwa.
- Kupanua vituo vya "Intership" toka vine (4) vya awali hadi kumi na sita (16) katika mwaka 2005/2008 na hivyo kuondoa kabisa mlundikano wa madaktari wanaosubiri kuanza "Intership".
- Baraza kwa kushirikiana na Mabaraza mengine ya Afrika, kupitia chama cha Mdaktari katika Afrika (AMCOA) limeandaa Protokali katika Nyanja zifuatazo;
  -Elimu ya kujiendeleza .
  -Masuala ya nidhamu katika taaluma.
  -Vigezo vya kusimamishwa kufanya kazi za taaluma kutokana na kupoteza uwezo (Professional Impairement)
  -Kuendesha Mafunzo ya Intership.

2.3.3.6 Baraza la Maabara

- Sheria mpya, Na. 22 ya mwaka 2007 inayohusika na Usajili wa Wataalamu wa Maabara imeundwa na kupata kibali cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Tanzania, mwezi Januari 2008.

2.3.3.7 Baraza la Radiolojia

- Sheria mpya, Na. 21 ya mwaka 2007 inayohusika na Usajili wa Wataalamu wa Radiolojia imeundwa na kupata kibali cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Tanzania, mwezi Januari 2008.

2.4 KINGA

Idara katika kipindi cha miaka mitatu imeendelea kuimarisha huduma zake katika nyanja zifuatazo; afya ya mazingira, huduma za mama na mtoto, kudhibiti

magonjwa ya kuambukiza yakiwemo ya milipuko kama vile Kipindupindu, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Malaria, Macho, Usubi, Malale na Tauni.

Mafanikio

2.4.1 Huduma za Afya na Usafi wa Mazingira

- Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa sheria ya afya ya jamii (Public Health Act), imepitia hatua zote na itawasilishwa katika kikao cha Bunge Januari 2009.

- Mpango Mkakati wa Afya na Usafi wa Mazingira umeandaliwa. Nia ya mpango huu ni kuinua kiwango cha usafi wa mazingira nchini na kutekeleza malengo ya MKUKUTA na MILENIA na utasaidia kudhibiti magonjwa kama vile kipindupindu.

- Wizara imehamasisha wilaya kuanzisha vijiji bora vya makazi kila mkoa na wilaya, ambavyo vinazingatia makazi bora, ikiwemo ujenzi wa nyumba na vyoo bora, uhakika wa kupata maji safi na salama, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira viwanja vya makazi vilivyopimwa na vyenye huduma nyingine muhimu. Vijiji vitano vimeanza mpango huo ambavyo ni, Namalenga, Masasi, Chumwi, Musoma Vijijini, Mkowe, Sumbawanga Vijijini, Kitisi, Iringa Vijijini na Kitunda, Ilala.

- Miongozo na viwango vya kudhibiti taka kutoka katika hospitali imeandaliwa na kusambaza katika wilaya zote nchini. Hali hiyo imewezesha kuboresha mifumo kwa kujenga matanuru (incinerators) bora ya kuteketeza taka katika hospitali 11 za mikoa na 69 za wilaya.

- Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Afya ya Mazingira [The Environmenta Health Practitioners (Registration) Act, 2007] imepitishwa.

2.4.2 **Udhibiti na ufuatiliaji wa Magonjwa (Epidemiolojia**)

- Taarifa za magonjwa nane ya kuambukiza na mlipuko ya kila wiki (Kipindupindu,tauni,surua, homa ya uti wa mgongo,kichaa cha mbwa,kupooza kwa ghafla, lishe ya watoto chini ya umri wa miaka mitano na vifo vya akina mama wajawazito), inapokelewa kutoka mikoa yote ya Tanzania bara na kutathiminiwa katika ngazi zote za utoaji huduma kwa lengo la kudhibiti na kupunguza athari na usambaaji wa magonjwa husika.Pia kutoa taarifa ya nchi ngazi ya kimataifa kulingana na mkataba wa utoaji taarifa,kupitia Shirika la Afya Duniani

- Wizara imefanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege ambapo vituo viwili vimeanzishwa katika wilaya ya Kibondo (Kigoma) na Mwananyamala(Dar Es Salaam).Sampuli huchukuliwa na kupelekwa kwenye maabara ya kitaifa kwa ajili ya uchunguzi wa vimelea vya ugonjwa huo.
- Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya (NIMR, CDC, AFENET, MUHAS, WHO) imeanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani ya Epidemiolojia na Maabara (Epidemiology and Laboratory Management).
- Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam wa afya ngazi ya Wilaya, kuhusu mbinu mpya za ufuatiliaji wa milipuko (Outbreak investigation and response). Mafunzo haya yametolewa katika wilaya 70 za Tanzania bara.

2.4.3 Mpango wa Kudhibiti Malaria

- Kuandaa, kupitishwa, kufundisha na kuanza kutumia mwongozo mpya wa kutibu Malaria, kwa kutumia dawa ya mseto aina ya Artemether/Lumefantrine (Alu) kuanzia Desemba 2006, na zinapatikana wakati wote katika vituo vyote vya huduma ya Afya vya Serikali, Dini, Majeshi na mashirika mbalimbali.

- Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa ajili ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria umetoa fedha kiasi cha dola za kimarekani 90.468 milioni kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya manunuzi ya dawa mseto na kuelimisha watoa huduma wote nchini.Dawa hizo zinatolewa katika vituo vya matibabu 4,921.

Wamiliki/aina ya kituo	**Hospitali**	**Kituo cha Afya**	**Zahanati**	**Jumla**
Serikali	89	346	3,550	3,985
Mashirika ya kujitolea	87	85	508	680
Mashirika ya Umma/Jeshi	8	12	236	256
Jumla	184	443	4,294	4,921

- Kwa kushirikiana na sekta binafsi wanawake wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kote nchini wanao hudhuria kliniki ya mama na mtoto wanapata chandarua chenye viuatilifu kwa bei nafuu, kwa Mpango wa Hati Punguzo. Hadi mwezi wa Novemba 2008, zaidi ya akina mama wajawazito milioni tatu kati ya makadirio ya walengwa milioni nne na laki nane wamepata vyandarua vyenye uatilifu kwa kupitia mpango huu.

- Kubuni, kuandaa na kuanza kutekeleza mpango maalum wa kusambaza vyandarua milioni 7.2 vyenye viatilifu vya muda mrefu katika kampeni maalumu kwa awamu kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Hadi sasa, watoto 117,000, sawa na asilimia 84 wenye umri chini ya miaka mitano, wamepata vyandarua katika Wilaya ya Mpanda mwezi wa Oktoba 2008 Iliyozinduliwa na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Kayanza Pinda, (Mb) na watoto 349,641, sawa na asilimia 90.4, walipata vyandarua katika mkoa wa Tanga wakati wa Kampeni ya Surua iliyofanyika mwezi Agosti 2008 iliyozinduliwa na makamu wa Rais, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein

- Mpango wa Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria umepitisha, mwezi Novemba 2008, kiasi cha Dola za Kimarekani 113,000,000 kwa ajili ya kuwezesha kila kaya ipate vyandarua viwili vyenye viatilifu kwa ajili ya kinga dhidi ya Malaria.

- Mpango wa kunyunyizia viuatilifu vya aina ya ICON majumbani**,** ambapo asilimia 90 ya kaya zilinyunyiziwa viuatilifu, hapo Juni, 2007 na Januari 2008, umeweza kuzuia milipuko ya malaria katika mkoa wa Kagera, hususani wilaya za Muleba na Karagwe.

2.4.4 UKIMWI:

- Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Desemba 2008, kumekuwa na ongezeko la huduma katika maeneo mbalimbali za kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kama inavyoainishwa katika jedwali:

Aina ya Huduma	**2005**	**2008**
Idadi ya vituo vinavyopima Virusi vya UKIMWI kwa hiari	515	1,643
Idadi ya watu waliopima virusi vya UKIMWI	2,000,000	6,836,450

kwa hiari		
Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo	96	400
Idadi ya wagonjwa wanaopata tiba na matunzo	100,000	377,155
Idadi ya wagonjwa wanopata dawa za kutibu UKIMWI	23,951	189,050
Idadi ya vituo vinavyotoa hudumaya kuzuia maambukizo ya UKIMWI kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto	544	2,474

- Ongezeko kubwa la waliopima kwa hiari virusi vya UKIMWI limetokana na Kampeni ya Kitaifa iliyozinduliwa na kuongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mh. Jakaya Mrisho Kikwete na mke wake Mama Salma Kikwete hapo tarehe 14 Julai 2007.

- Asilimia 34 ya wanawake wote wajawazito wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI walipata dawa za kuzuia maambukizi hayo yasiende kwa watoto wao.

- Viwango vya maambukizi ya virusi vya UKIMWI hapa nchini vimeshuka kutoka wastani wa asilimia 7 mwaka 2005 kufikia asilimia 4.8 mwaka 2008, kufuatia kampeni ya kitaifa ya upimaji wa hiari.

- Wizara imeandaa Mpango Mkakati mpya wa Kisekta wa kudhibiti UKIMWI wa kipindi cha miaka mitano 2008-2012. Mpango huo unalenga kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu za kudhibiti na kutibu UKIMWI nchini.

- Mkakati wa Kuzuia Maambukizi mapya ya VVU/ UKIMWI kwa wafanyakazi wa sekta ya Afya, umetayarishwa na kuzinduliwa mwaka 2007, na umeanza kutumika.Pia miongozo na nyenzo za kufundishia masuala ya UKIMWI sehemu za kazi, zimeandaliwa na zinatumika.

2.4.5 Kifua Kikuu na Ukoma

Matibabu ya Kifua Kikuu yameboreshwa kwa kupunguza idadi ya vidonge kutoka 12 hadi 3 kwa siku, ambazo ni dawa mpya za mseto (Fixed Dose Combination). Pia kipindi cha matibabu kimepungua kutoka miezi 8 hadi 6. Kumekuwa na ongezeko la vituo vilivyowezeshwa kutibu kwa dawa mseto kama ifuatavyo.

Ngazi ya huduma	**Mwaka 2005**	**Mwaka 2008**
Hospitali	185	203
Vituo vya Afya	450	628
Zahanati	1,000	2,218
Jumla	1,635	3,049

- Kati ya mwaka 2005 hadi mwaka 2008 vituo vyote vya huduma vilikuwa na dawa za Kifua Kikuu na Ukoma za kutosha. Huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI, kwa sasa zimefika katika wilaya zote 132 , ukilinganisha na wilaya 3 hapo mwaka 2005. Hadi kufikia mwezi Septemba 2008, asilimia 81 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa wamepima damu ili kubaini hali ya uambukizo wa virusi vya UKIMWI na kupatiwa matibabu.

- Taifa limefikia kiwango cha chini cha utambuzi wa mgonjwa 1 kati ya watu 10,000 katika kutokomeza ugonjwa wa Ukoma. Hivyo kwa kufuatana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani,**Ukoma si tatizo tena la afya ya jamii hapa Tanzania**. Viwango hivi vilifikiwa mwaka 2007 na Tanzania imepata tuzo kutokana na mafanikio haya.

2.4.6 Magonjwa yanayoenezwa na wadudu wadhurifu:

- Ufuatiliaji (Surveillance) ulifanyika wa viashiria vya ugonjwa na kazi za udhibiti wa homa ya malale mkoani Tabora, wilayani Urambo umeweza kudhibiti ugonjwa wa malale katika wilaya hiyo.

- Mlipuko wa ugonjwa wa tauni katika wilaya ya Lushoto umedhibitiwa katika kipindi cha miaka 3, kuanzia mwaka 2005 hadi 2008.

-

2.4.7 Afya ya uzazi na mtoto

2.4.7.1 **Uzazi Salama**

- Huduma kwa wanawake wajawazito, kujifungua, chanjo, matibabu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na huduma za uzazi wa mpango zimeendelea kutolewa kwa gharama za serikali katika vituo vyote vya serikali vya kutolea huduma za afya nchini.

- Mpango mkakati wa miaka saba(2008-2015) wa kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto umeandaliwa na kuzinduliwa rasmi na mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu wa Norway Mhe. Steltenberg, mwezi Aprili 2008. Mpango huu unatekelezwa na wadau mbalimbali, na unalenga kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

- Miongozo mbalimbali imeandaliwa ili kuboresha utoaji huduma.Miongozo hiyo ni, Mwongozo wa kutathimini vifo vya wanawake wajawazito, mwongozo kwa mtoa huduma uzazi salama, mwongozo wa namna ya kumhudumia mama wakati wa kujifungua ili kuepuka kupoteza damu nyingi pamoja na mtaala wa mafunzo ya stadi za kazi kuhusu uzazi salama.

- Mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma ya Afya kuhusu uzazi salama yametolewa mikoa yote Tanzania bara jumla ya watoa huduma 2,379 wamepata mafunzo haya

- Watoa huduma 330 wamepata mafunzo ya jinsi ya kumhudumia mwanamke anapopata tatizo la kuharibu mimba.

- Wizara kwa kushikiana na wadau imenunua magari 6 kwa ajili ya kubebea wagonjwa katika wilaya za Mafia, Kibaha, Ruangwa, Tukuyu, Mpanda na Nkasi. Ushirikiano wa wadau umeimarika hasa katika ngazi ya taifa kwa kuwepo kwa mfumo wa kukutana, kupanga, kubadilishana uzoefu na utaalam wa utekelezaji wa masuala ya afya na maendeleo ya vijana

- Kumekuwa na ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vinatoa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana kwa asilimia 30 kutoka asilimia 5 ya mwaka 2005.

2.4.8 Uzazi wa Mpango

- Serikali kwa kushirikiana na wadau imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango kwa wakati katika wilaya zote na kwa kipindi chote hakukuwa na uhaba wa dawa hizi hapa nchini.

- Mitaala ya kufundishia waalimu wa Uzazi wa Mpango (TOT), kitita cha mtoa huduma cha Uzazi wa Mpango na miongozo ya kwa ajili ya watoa huduma katika jamii (CBD) imepitiwa upya na kuboreshwa.

2.4.9 Mpango wa Taifa wa Chanjo

- Viwango vya chanjo zote vimebaki kuwa zaidi ya asilimia 80% na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano.

- Wizara imeendesha kampeni ya surua kwa watoto wote nchini wenye umri kati ya miezi 9 mpaka miaka 10 tangu tarehe 30 Agosti hadi 1 Septemba 2008. Jumla ya watoto 10,567,104 walipatiwa chanjo hii. Aidha, chanjo ya polio ilitolewa katika wilaya 18 za mipakani na zenye viashiria vya kuambukiza polio. Jumla ya watoto 1, 459,162 walipata chanjo hii.

- Viwango vya chanjo ya polio vimefikia zaidi ya asilimia 90 na mgonjwa wa mwisho wa polio hapa nchini alipatikana mwaka 1996 Julai.

- Pikipiki 121 zimenunuliwa na kusambazwa katika halmashauri husika ili kuboresha huduma za chanjo na afya kwa jumla.

- Jumla ya majokofu 1,722 yanayotumia nishati ya gesi na mionzi ya jua yamesambazwa katika maeneo yasiyo na nishati ya umeme kwa ajili ya kuhifadhia chanjo

2.4.10 Udhibiti wa magonjwa ya Watoto kwa Uwiano

- Serikali imewezesha halmashauri zote kutekeleza mpango wa udhibiti wa magonjwa ya Watoto kwa Uwiano (IMCI) ili kuboresha matibabu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

- Vitabu, miongozo ya mafunzo na vielelezo mbalimbali vilichapishwa na kusambazwa katika wilaya: Miongozo na vielelezo vilivyotayarishwa ni:

    - Mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya utunzaji wa watoto wachanga wenye uzito pungufu (Kangaroo Mother Care Guideline).

    - Miongozo ya mafunzo kwa ajili ya utunzaji wa watoto wachanga (Essential Newborn Care).

- Nakala 6,000 za miongozo ya kufundishia (training modules), nakala 8,000 za vitabu vya mazoezi (exercise modules), nakala 1,000 za mwongozo wa IMCI pamoja na vijarida vilichapishwa na kusambazwa nchini.Pia vipeperushi vinavyoonesha mabadiliko mapya ya matibabu ya mtoto vimeandaliwa na kusambazwa.

2.4.11 **Huduma ya Udhibiti wa Saratani**

- Vituo 33 vya kupimia wanawake saratani ya matiti na shingo ya kizazi vimeanzishwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Dododma, Lindi, Pwani, Tanga, Mwanza, morogoro, Ruvuma, Kilimanjaro na Iringa.

- Kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), wanawake zaidi ya 63,895 wamechunguzwa kutambua dalili za saratani ya matiti kupitia kampeni zilizofanyika mikoa 7 ya Dar es Salaam Mbeya, Mwanza, Lindi, Mtwara, Manyara na Dodoma.

- Kupitia kampeni hizo, asilimia 4 ya wanawake 2978 waliopatikana na matatizo ya matiti, walikuwa na saratani na walipatiwa matibabu katika vituo vya tiba vya Serikali.

- Kwa kushirikiana na wadau kutoka Marekani, mashine 5 za kuchunguza matiti “Mammograph machine” zilipatikana na kuwekwa katika hospitali za Lindi, Kibaha, Amana, Ocean Road na Arusha.

2.4.12 Huduma ya Afya ya Msingi katika Jamii

- Usimamizi na ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa katika ngazi ya jamii umefanyika katika Mikoa 14 na Halmashauri 38 Mikoa ya Mbeya, Lindi, Tabora, Manyara, Mwanza, Morogoro, Kagera, Iringa, Dodoma, kilimanjaro, Tanga, Mtwara na Pwani. Halmashauri za Kyela, Rungwe na Mbozi. Rwangwa, Nachingwea na Lindi. Urambo, Sikonge na Uyui. Mbulu, Babati na Karatu. Sengerema, Geita, na Kwimba. Kilosa Morogoro na Mvomero. Bukoba na Muleba. Njombe, Ludewa na Makete. Kongwa, Kondoa na Chamwino. Hai, Mwanga na Halmashauri ya wilaya ya Moshi. Manispaa ya Tanga, Muheza na Mkinga. Mtwara, Tandahimba Newala. Rufiji, Kisarawe na Mkuranga. Lushoto, Muheza na Korogwe.

2.4.13 Huduma ya Macho:

- kwa kushirikiana na wadau wa huduma za macho Mpango Kabambe wa kitaifa wa Huduma za Macho wa miaka mitano 2009 – 2013 umendaliwa na kupitishwa
- Kwa kushirikiana na wadau umetengenezwa mpango kabambe wa miaka mitano, (2008-2012) wa udhibiti wa ugonjwa wa Vikope [Trachoma], katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

- Kazi ya uwezeshaji Mikoa na Halmashauri kujenga uwezo na mazingira ya jamii kushiriki katika masuala ya Afya ya Macho imefanyika katika mikoa 21 ya Tanzania bara.
  - Kufanya utafiti wa ugonjwa wa usubi nchini ambapo wilaya ya Mufindi na Njombe ziligundulika kuwa na kiwango kikubwa cha ugonjwa.
  - Tathimini ya kuangalia uendelevu wa Miradi ya Usubi katika mikoa ya Morogoro na Ruvuma ilifanyika kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani(WHO),ambapo halmashauri zimeanza kuingiza shughuli za kudhibiti Usubi katika Mipango Kabambe ya Wilaya (CCHP)
  - Mpango Mkakati wa kutokomeza Usubi wa miaka mitano wenye lengo la kutokomeza ugonjwa wa usubi hapa nchini umekamilika., umeandaliwa na uko katika hatua za mwisho za kukamilishwa.

2.4.14 Huduma za afya shuleni

- Kampeni ya kugawa dawa ya kichocho (Praziquantel) na dawa ya minyoo (Albendazole/Mebendazole) kwa wanafunzi wa Shule za Msingi imefanyika katika Mikoa 17. Mikoa 11 ilitoa mzunguko wa kwanza wa dawa hizo mwaka 2005 na kurudia mwaka 2007. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Lindi, Mtwara, Mwanza, Mara, Kagera, Tabora, Shinyanga na Kigoma. Wanafunzi walengwa waliopata dawa 2005 ni 78% na 2007 ni 85%. Mikoa 6 zaidi imetoa mzunguko wa kwanza wa dawa mwaka 2008. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Morogoro na Rukwa. Wanafunzi walengwa waliopata dawa ni zaidi ya Asilimia 70.

2.4.15 Huduma za Elimu ya Afya kwa Umma

- Wizara inaendelea kuelimisha wananchi njia za kujikinga na kudhibiti maradhi kupitia njia mbalimbali zikiwemo vipindi vya redio, magazeti na Televisheni. Jumla ya Vipindi vya redio 208 vya “Siri ya Afya Bora” vilirushwa hewani na mada

zilizohusika ni; umuhimu wa maji na usafi wa mazingira, makazi na vyoo bora, mazoezi ya viungo, lishe bora, afya shuleni, uzazi salama, unyonyeshaji bora, umuhimu wa chanjo, matumizi sahihi ya dawa, damu salama.na tiba asili. Aidha mada nyingine zilizoongelewa kwenye vipindi hivyo vya redio ni namna ya kujikinga na maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Malaria, Kipindupindu, Magonjwa ya kuharisha, homa ya matumbo, magonjwa ya utotoni, magonjwa ya macho na upofu, Kichaa cha mbwa, Kifafa, Kisukari, madhara ya tumbaku, Saratani, Homa ya uti wa mgongo, Homa ya Bonde la Ufa, Ebola na Homa ya Mafua ya ndege

- Vielelezo mbalimbali vilisambazwa vikiwemo vipeperushi na mabango ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kujikinga na maradhi yakiwemo homa ya bonde la ufa, mafua ya ndege, kichaa cha mbwa, kipindupindu, homa ya matumbo, kisukari, umuhimu wa mazoezi ya viungo kwa afya na madhara ya tumbaku.

- Kuanzishwa kwa mtandao wa waandishi wa habari wa masuala ya afya, (Tanzania Health Writers' Network) ya kuwawezesha kutoa taarifa sahihi kuhusu afya ya jamii.

2.5 TIBA

Inashughulikia huduma za utoaji matibabu, kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, rufaa ya mkoa, na hospitali maalum, za serikali na binafsi, kwa matibabu ya nje na ya ndani. Katika vituo hivyo huduma zifuatazo hutolewa; uchunguzi, dawa, vifaa tiba na rufaa.

2.5.1 Matibabu

Mafanikio

Orodha ya vituo vya Serikali

Ngazi	2006	2008
Zahanati	3,619	4,589
Vituo vya Afya	373	481
Hospitali za Wilaya	57	58
Hospitali za Taasisi	3	6
Hospitali za Rufaa -Mkoa	18	21
Hospitali Maalum	4	4
Hospitali za Kanda	2	2

2.5.2 Afya ya Kinywa

Uimarishaji wa huduma za afya ya kinywa unapewa kipaumbele na kuwa na mafanikio yafuatayo:

- Vituo 270 vya kutolea huduma ya dharura ya tiba ya meno (Emergency Oral Health Care) vimeanzishwa nchi nzima.
- Tabibu 270 wa vituo hivyo wamepewa mafunzo maalum ya jinsi ya kutoa huduma za kinywa pamoja na kupatiwa vifaa vya matibabu.
- Kuwekwa vifaa vya tiba ya meno (Dental Equipment) katika halmashauri 91.

2.5.3 Mashirika ya Kujitolea na Binafsi (Voluntary and Private Organizations)

Serikali imeendelea kusimamia na kuratibu huduma za afya zinazotolewa na mashirika ya kujitolea, na watu binafsi.

Mafanikio

Orodha ya vituo Binafsi

Ngazi	**2006**	**2008**
Zahanati	1,704	1,873
Vituo vya Afya	153	182
Hospitali za Wilaya/ teule	21	25
Hospitali za Kawaida (VA)	92	96
Hospitali za Rufaa-Mkoa	18	21
Hospitali Maalum	1	1
Hospitali za Kanda	2	2

- Kutayarisha na kukamilisha mkataba maalumu wa utoaji huduma kati ya Halmashauri na vituo vya matibabu binafsi (Service Agreement) kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

- Serikali imeongeza ruzuku kwa kitanda kwa mashirika ya kujitolea/dini kutoka shilingi 15,000 kwa kitanda hadi shilingi 50,000 kwa kitanda kwa mashirika ambayo yanatoa huduma katika maeneo ambayo serikali haina vituo vya kutolea huduma.

2.5.4 Uchunguzi wa Magonjwa

Huduma za uchunguzi wa magonjwa unajumuisha huduma za maabara, radiolojia, ufundi wa vifaa tiba, kwa wagonjwa na uchunguzi wa vifo vinavyotokana na makosa ya jinai, mauaji au vifo vya ghafla.

2.5.5 Huduma za Maabara na Ufundi wa Vifaa Tiba

Mafanikio

- Maabara zote za Rufaa na Mikoa zimepewa mashine za kuchunguza damu na uwezo wa figo na ini pamoja na chembe chembe za kinga – CD4 kwa ajili ya uanzishwaji na ufuatiliaji wa matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI.

- Maabara zote za Wilaya zimepewa mashine za kuchunguza damu na uwezo wa figo na ini kwa ajili ya ufuatiliaji wa matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI.

- Maabara zote za Kanda zimepewa mashine maalum (DNA PCR) kwa ajili ya kuchunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU) kwa watoto wachanga chini ya miezi 18.

- Maabara zote za Kanda ziko kwenye mchakato wa kurasimishwa kwenye Ithibati ya viwango vya kimataifa vya ubora wa huduma za maaabara (Laboratory Accreditation On International Standards).

- Maabara ya Taifa ya Afya za Jamii imejengwa katika eneo la NMR/CDC. Maabara hii, itahusika na uchunguzi wa magonjwa ya milipuko ikiwemo

homa ya bonde la ufa pamoja na kusimamia na kutoa mafunzo ya uhakiki wa ubora wa huduma za Maabara (Laboratory Quality Assurance).

- Utaratibu wa kitaifa wa upimaji wa haraka wa VVU (National HIV rapid testing algorithm umebadilishwa kutoka utaratibu wa 'Capillus' iliyohitaji kutunzwa kwenye ubaridi na kutumia utaratibu wa 'SD Bioline usiyohitaji kutunzwa kwenye ubaridi.

- Maabara za hospitali za Rufaa (2) za Mikoa (2) zimepewa jumla ya Komputa 37, Bugando (14), Mbeya Rufaa (11), Shinyanga (5) Ruvuma (5) na Wizara (2) kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa taarifa za Maabara kwa njia ya komputa (Electronic Laboratory Information System).

- Shule za wataalamu wa Maabara ngazi ya Cheti (Laboratory Assistants) zimeongezeka kutoka 3 hadi 5.

- Mafunzo ya shahada kwa wataalamu wa Maabara yameanzishwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili.

- Mtaala ya vyuo vya Maabara vya ngazi ya Stashahada (Diploma in Medical Laboratory Sciences) umepitiwa na kurekebishwa ili kuingiza elimu ya upimaji wa maambukizi ya VVU, uhakiki wa ubora wa vipimo vya maabara naMenejimenti ya huduma za maabara.

- Mafunzo ya kujiendeleza na ya muda mfupi kwa wataalamu wa maabara kuhusu uchunguzi wa magonjwa na utumiaji wa vifaa vya kisasa vya Maabara yametolewa katika mikoa na wilaya zote.

- Mchakato wa mafunzo ya Stashahada ya ufundi wa vifaa tiba umeanzishwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Ufundi ya Dar es Salaam. Mtaala umekamilika na mkutano wa wadau umeshafanyika. Udahili wa wanachuo wa ufundi wa wa vifaa tiba utafanyika Septemba, 2009.

2.5.6 Huduma za Radiolijia

Huduma za radiolojia ni pamoja na x-ray,ultrasound,CT Scanner na MRI "Magnetic Resonance Imaging",.

Mafanikio

- Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepatiwa “Magnetic Resonance Imaging” - (MRI), mashine nne za ultra sound katika hospitali za kanda na kulipia gharama zote za mashine ya x-ray kwa ajili ya wilaya tatu za mkoa wa Dar es Salaam, pamoja na wilaya za Chato (Kagera), Tandahimba (Mtwara) Bukombe (Shinyanga), kwa ushirikiano na Serikali ya Uholanzi kupitia mradi wa “Overseas Related Export Trade – ORET”.

- Wizara ilianzisha mpango wa kitaifa wa upatikanaji wa Damu Salama, nchi nzima na kwa sasa kuna vituo sita vya Kanda vinavyofanya kazi. Vituo hivi viko Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kaskazini (Kilimanjaro), kanda ya Ziwa (Mwanza) na Kanda ya Mashariki Makao Makuu (Dar es Salaam), Kanda ya Magharibi, Tabora na Kanda ya Kusini, Mtwara.

- Karakana tano (KCMC, BMC, MNH, MRH na Ligula Mtwara) za kanda za matengenezo ya vifaa tiba zimeboreshwa kwa kupatiwa nyenzo na magari na pia mafundi wamepewa mafunzo maalumu. Vifaa tiba katika kanda hizo kwa hivi sasa vinahudumiwa na kufanya matengenezo ya kinga.

2.5.7 Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba

Mafanikio:

- Jumla ya zahanati za Serikali na Binafsi zinazopewa dawa na vifaa tiba zimeongezeka kutoka … mwaka 2005 mpaka 3,619 mwaka 2008 na vituo vya afya vya Serikali na binafsi kutoka … mwaka 2005 mpaka 373 mwaka 2008 vimepewa dawa na vifaa tiba.

- Kuanza kutumia mfumo wa “Indent/Integrated system (ILS)” wa uagizaji wa dawa kulingana na mahitaji na mgao wa fedha kwenye vituo vya Serikali vya kutolea huduma za afya badala ya “Kit system” nchi nzima. Mikoa 15 inatumia ILS na mikoa 6 inatumia indent.

- Kusimamia uagizaji na usambazaji dawa za programu maalum za Malaria (ALU), UKIMWI (ARVs), Kifua Kikuu na Ukoma, Vikope na Matende na kuhakikisha zinapatikana wakati wote kwenye vituo.

- Kuandaa , kukamilisha na kupitishwa orodha ya Dawa Muhimu (Essential Drugs List) pamoja na mwongozo wa kutibu magonjwa muhimu (Standard Treatement Guidelines) ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora

- Kuandaa, kufuatilia na kusimamia upatikanaji wa fedha za kununua dawa, vifaa na vifaa tiba kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo mfuko pamoja(Basket fund),Mfuko wa dunia wa magonjwa maalum (Global fund) na Mfuko wa dunia wa chanjo(GAVI).

2.5.8 Afya ya Akili na Madawa ya Kulevya

- Kukamilisha mkakati wa Taifa wa huduma za afya ya akili 2006.
- Sheria ya Afya ya akili ya mwaka 2008, imepitishwa
- Kuanzishwa huduma ngazi ya msingi katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Mwanza, Shinyanga na Tanga.
- Madaktari 22 wamepatiwa masomo ya muda mfupi wa na kutibu wagojwa wa akili katika hospital za mikoa na wilaya.
- Ujenzi wa kituo maalum cha matibabu na utengemao (Rehabilitation services) wa waathirika wa pombe na vilevi vingine, unaendelea eneo la Mirembe, Dodoma.

2.5.9 Magonjwa yasiyoambukizwa

- Mkakati wa Taifa wa huduma za magonjwa yasiyombukiza umekamilishwa mwaka 2008.

2.5.10 Tiba Asili na Tiba Mbadala

- Kufanikisha kuwa na kongamano la “African Traditonal Day,” kila mwaka.
- Mwongozo wa kufundishia waganga wa Tiba Asili umeandaliwa.

2.5.11 Rufaa na Wagonjwa wa Nje

- Kwa mwaka 2008, wagonjwa 741 kati ya wagonjwa 1,727 walipelekwa kutibiwa nje ya nchi. Serikali imeongeza fedha za kutibu wagonjwa nje kufikia Bilioni 4 kwa mwaka 2008.

- Kuanzishwa kwa huduma za Upasuaji mkubwa wa moyo kwenye hospital ya Taifa ya Muhimbili na kuanza kutoa huduma za upasuaji na uwekaji viungo bandia vya nyonga na goti (hip and knee replacement), katika taasisi ya MOI hapa nchini, ili kupunguza gharama ya kepeleka wagonjwa nje ya nchi

2.6 MAFUNZO

Idara ya Mafunzo inaratibu na kusimamia mipango na mafunzo ya wataalamu katika sekta ya afya nchini, kwa kutumia vyuo 74 vinavyomilikiwa na Serikali na kuratibu vyuo 42 vinavyomilikiwa na mashirika ya dini na binafsi.

Mafanikio

2.6.1 Mipango ya Watumishi wa afya

- Kutayarisha, kukamilisha na kuanza kuutumia Mpango Mkakati wa Watumishi wa afya (2008- 2013), unaotoa dira na kuweka malengo ya kuboresha maendeleo na matumizi ya rasilimali watu katika sekta ya afya.
- Kukamilisha maandalizi ya kujumuisha taarifa za watumishi wa afya katika mfumo wa taarifa za uendeshaji wa huduma afya nchini (MTUHA). Ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za rasilimali watu katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma.

2.6.2 Elimu Endelevu

- Kuandaa, Kukamilisha na kupitishwa kwa Mpango wa Elimu endelevu wa watumishi wa afya nchini. Ambapo mafunzo yamekwishatolewa katika ngazi ya mikoa na halmashauri zote
- Kuandaa na kukamilisha moduli za mafunzo ya kujiendeleza katika ngazi ya kituo cha afya na zahanati. Mafunzo yameanza katika wilaya……..
- Kufanyika kwa tathimini ya mafunzo ya kujiendeleza kwa njia ya masafa marefu nchini, ili kuboresha mafunzo endelevu kwa watumishi wa kada zote za afya.
- Kuandaa,kukamilisha na kuanza kutumia kwa moduli ya uendeshaji huduma ngazi ya wilaya (District Health Management),mafunzo hayo yameanza katika kanda nne kati ya nane.
- Kuongeza wanafunzi wa mafunzo ya uzamili wanaolipiwa na Serikali. Kutoka wanafunzi 56 kwa Mwaka 2005 mpaka148 mwaka 2008,hili ni ongezeko la asilimia 164.

MWAKA	2005	2006	2007	2008
WANAFUNZI WA UZAMILI	56	61	130	148

2.6.3 Sayansi Shiriki na Uuguzi

- Serikali imefanikio kuongeza wahitimu wa mafuzo mbalimbali toka 2,858 katika mwaka 2005 hadi kufikia 3,038 katika mwaka 2008 wa kada za afya zifuatazo Madaktari Wasaidizi,Tabibu, Maafisa Afya, Mafundi Sanifu Maabara, Madawa,Macho na Wauguzi.
- Serikali pia imeongeza wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya kutoka 1,013 mwaka 2005 kufikia 3,831 mwaka 2008. Ongezeko hili la asilimi (278%).Ongezeko hili litaiwezesha Serikali kupata mafanikio katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM).

MWAKA	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**
IDADI YA WANAFUNZI WATARAJALI WALIODAHILIWA SAYANSI SHIRIKI	493	497	575	1,520
IDADI YA WANAFUNZI WATARAJALI WALIODAHILIWA UUGUZI	520	611	745	2,311
JUMLA	1,013	1,108	1,320	3,831

- Kupitia na kukamilisha mitaala 6 na kuiboresha na pia kupunguza muda wa mafunzo darasani kwa mwaka mmoja kwa baadhi ya kada.Mitaala hiyo ni ya Wazoeza Viungo,Tabibu , Tabibu Wasaidizi,Mafundi Sanifu Macho na Wauguzi.
- Kurudishwa kwa mafunzo ya kada ya Tabibu Msaidizi na “MCHAider” kwa ajili ya zahanati na kutumia muda mfupi wa mafunzo ya miaka miwili. Awali kozi hii ilikuwa inafunzwa kwa muda wa miaka mitatu.
- Vyuo vya afya vipatavyo 93 vimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na 45 vipo katika hatua mbalimbali za kupata ithibati.

2.7 USTAWI WA JAMII

2.7.1 Huduma ya Watu wenye Ulemavu na Wazee

- Kuandaa muswada wa Sheria jumuishi ya watu wenye ulemavu na wasiojiweza “Disability Bill”, ili kuzibadili sheria Namba 2 ya ajira na Sheria Namba 3 ya Matunzo kwa Watu Wenye Ulemavu na Wasiojiweza.
- Serikali kusaini mkataba wa Kimataifa juu ya haki ya watu wenye ulemavu.
- Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inakusanya takwimu ili kubaini mahitaji ya watu wenye ulemavu.
- Serikali imeunda na kuzindua kamati ya kitaifa ya Muongo wa Watu Wenye Ulemavu mnamo mwezi Julai 2008.
- Serikali iligharamia timu ya wadau 7 wakiwemo Askari, Waandishi, Maafisa Ustawi jamii na Viongozi wa Chama cha Maalbino kwenda katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa lengo kutambua chanzo na ukubwa wa tatizo la vitendo vya ukatili na mauaji ya maalbino.
- Kufanikiwa kutumia fursa ya maadhimisho ya siku ya kitaifa ya watu wenye ulemavu kukemea vitendo vya ukatili na mauaji ya maalbino.
- Jumla ya vituo 51vya huduma za ustawi wa familia na watoto na malezi ya awali kwa Watoto Wadogo vya mashirika ya dini na binafsi vimeongezeka.

2.7.2 Ustawi wa Familia

- Huduma ya ushauri nasaha na kusuruhisha ndoa zenye migogoro.Jumla ya familia 2,250 zilipata huduma hiyo.
- Serikali ilitoa misaada ya dharura kwa familia 450 zisizokuwa na uwezo na zilizoathirika na kuathiriwa na UKIMWI.

2.7.3 Ustawi na Maendeleo ya Mtoto:

- Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na TAMISEMI imeandaa Mpango kazi wenye makadirio (2007 – 2010) wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi (National Costed Plan of Action 2007 – 2010) ambao unatekelezwa na wadau mbalimbali, ambapo nakala 5,000 za mpango zimesambazwa.

- Kukamilisha na kuanza kutumia mwongozo wa uwezeshaji haki jamii kuwasaidia watoto walio katika mazingira hatarishi kupata haki za kisheria. Wawezeshaji 25,000 wamepatiwa mafunzo ya uwezeshaji haki jamii katika Halmashauri 26.

- Mpango wa utambuzi na huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi unatekelezwa katika Halmashauri 78 na jumla ya watoto 511,820 ambao wasichana ni 245,674 na wavulana ni 266,146 wametambuliwa. Kati ya watoto hao 432,322 wamepatiwa huduma mbalimbali. Huduma hizo ni pamoja na, vifaa vya shule,karo, kujengewa/kufanya ukarabati wa nyumba zao na walezi wao, msaada wa chakula na lishe, huduma za afya na ushauri wa kisaikolojia na msaada wa kisheria.

    - Maafisa Ustawi na watoa huduma 173 katika Halmashauri 53 wamepatiwa mafunzo ya kukusanya, kutunza na kutumia takwimu za watoto walio katika mazingira hatarishi.

2.7.4 Uratibu na Usimamizi wa Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi:

- Serikali imeandaa mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa makao ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi. Hadi kufikia Desemba, 2008 yapo makao 83 yaliyosajiliwa yanayohudumia watoto 3,238.

- Serikali imeandaa mwongozo wa malezi ya kambo na kuasili ambao unaelekeza namna ya kutoa huduma hiyo. Hadi kufikia mwaka 2008 Wizara ilipokea maombi ya malezi ya kambo 168 kati ya hayo 54 yamepata kibali na kati ya hayo watoto 36 wameasiliwa

Maombi/Watoto	2006	2007	2008
Maombi yaliyopokelewa	42	45	44
Maombi yaliyopata vibali	15	12	16
Watoto walioasiliwa mahakama kuu	12	7	9

2.7.5 Malezi ya Awali

- Mtaala wa mafunzo ya malezi ya watoto wadogo umepitiwa na kuingiza masuala mapya yanayohusu malezi kwa watoto wanaoishi na VVU na utambuzi wa awali kwa watoto wenye ulemavu.
- Serikali imeandaa mwongozo wa uwezeshaji wa malezi changamshi ya awali kwa watoto wadogo pamoja na makala mbalimbali za kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa malezi kwa watoto wadogo.
- Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mtandao wa Malezi Tanzania inatekeleza mpango jumuishi wa kutoa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto wadogo (Intergrated ECD Service Delivery) .
- Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 51 vimesajiliwa kati ya 180 vilivyowasilisha maombi, na kufanya idadi kufikia vituo 442.
- Mafunzo ya malezi ya watoto wadogo yametolewa katika vyuo 12, ambapo walezi 996 walipata mafunzo hayo.

2.7.3 Huduma za Marekebisho ya Tabia kwa Watoto na Vijana

- Kufanya ukarabati wa majengo ya mahabusi 5 za mkoa wa Arusha, Moshi,Tanga, Mbeya na Dar Es Salam na shule ya maadilisho 1 ya Mkoa wa Mbeya.

- Wizara imeandaa kitabu cha maadili ya maafisa majaribio na mkataba wa huduma kwa mteja (Code of Conduct na Customer Care Service).

2.8 Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

- Taasisi imeanzisha mafunzo ya Shahada katika fani za huduma ya Ustawi wa Jamii, Rasilimali Watu na Mahusiano,Stashahada za kawaida (Ordinary Diploma NTA Level 6),na masomo ya jioni katika mafunzo ya Shahada na Stashahada ya Uzamili ya Sheria , Usuluhishi na Uamuzi.

- Kumekuwa na ongezeko la wanafunzi toka 1,036 kwa mwaka 2005/06 hadi kufikia wanafunzi 2,496 kwa mwaka 2008/09 sawa na asilimia 141. Katika mwaka wa masomo 2008/09 idadi ya wanafunzi wa kiume ni 1,086 na wanawake ni 1,410 ambao ni asilimia 56 ya wanafunzi wote.
  •Yameanzishwa mafunzo ya “Para Social Workers” kwa ajili ya kuwahudumia watoto yatima wanaotokana na tatizo la UKIMWI. Mafunzo yanaendeshwa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Jane Addams School of Social Work- kutoka chuo kikuu cha Chicago,Illinois nchini Marekani na American International Health Alliance.

- Taasisi imeajiri walimu wengi kutokana na ongezeko la wanafunzi.

- Ujenzi wa maktaba ya kisasa unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka 2009/10.

2.9 FEDHA NA UHASIBU

Fedha na uhasibu inasimamia upokeaji,utunzaji na ulipaji wa fedha katika shughuli za afya na ustawi wa jamii kulingana na bajeti iliyopitishwa.

Mafanikio

- Kuboresha mfumo wa kupokea,kuweka kwenye mtandao,Kulipa na kutoa taarifa za fedha na utekelezaji wa bajeti kwa wakati, kwa kutumia mtandao wa malipo na fedha zilizowekwa hazina Integrated Financial Management System(IFMS).
- Ongezeko la ufanisi na udhibiti wa matumizi ya fedha kwa kutumia mfumo wa IFMS.

2.9.1 Utoaji wa taarifa za fedha na utekelezaji wa Bajeti

Wizara imeendelea kutoa taarifa hizi kwa wakati na hivyo kurahisisha ulinganishaji takwimu za miaka ya nyuma kwa kutumia mtandao wa malipo na Fedha zilizowekwa hazina (IFMS) kama inavyoainishwa kwenye jedwali

Jedwali: Malipo na Fedha zilizotolewa na Hazina

MATUMIZI YA KAWAIDA	BAJETI	GAWIO	MATUMIZI
2004-05	105.08	105.08	104.16
2005-06	171.59	152.81	150.87
2006-07	181.21	178.98	178.98
2007-08	192.88	174.05	173.22

BAJETI YA MAENDELEO	BAJETI	GAWIO	MATUMIZI
2004-05	91.22	72.31	71.71
2005-06	103.44	84.25	84.23
2006-07	96.30	94.72	94.72
2007-08	181.94	118.18	108.77





- Kwa Mwaka 2008 Wizara ilichukua ushindi wa kwanza kwa kutengeneza hesabu zake za mwaka zinazokidhi viwango vya kimataifa yaani International Public Sector Accounting Standard (IPSAS)

2.9.2 Ukusanyaji wa Mapato.

Kumekuwa na ongezeko la mapato halisi yatokanayo na uchangiaji huduma kwa kipindi cha kuanzia Desemba 2005 hadi Desemba, 2008 kutoka shilingi bilioni 1.3 hadi kufikia shilingi bilioni 2.1, kutokana na ada za mafunzo, usajili wa maabara binafsi na vifaa vya maabara, uandikishaji wa hospitali binafsi na uchangiaji huduma za matibabu.

2.9.3 Kulipa Mishahara, na malimbikizo

- Wakati wa ulipaji mishahara na marupurupu ya watumishi imeendelea, Wizara imeweka utaratibu wa kufuatilia watumishi waliopo mikoani ili kubaini kuwepo kwa watumishi hao ili kusaidia kuhakiki taarifa zinazopokelewa, pamoja na kusikiliza matatizo yao kwa lengo la kuharakisha haki za mtumishi zinapatikana.

2.9.4 Utekelezaji wa Maagizo ya Wakaguzi na Kamati za Bunge

- Wizara imetekeleza kikamilifu maagizo yote ya wakaguzi wa mahesabu ya fedha na Kamati za Bunge**.**

- Kupunguza hoja za Ukaguzi kwa zaidi ya asilimia 50% kutoka hoja 60 za Ukaguzi kwa mwaka 2004/2005 hadi kufikia hoja 23 kwa mwaka 2007/08.

- Ukaguzi maalum wa mtandao wa bohari kuu ya dawa (MSD) ulifanyika ili kuthibitisha ubora wa mtandao huo.

- Kuwaendeleza wataalamu wa masuala ya fedha katika eneo lao na kufanikiwa kupata wahitimu 13 wa ngazi mbalimbali za uhasibu.

2.10 UKAGUZI WA NDANI

- Kuimarisha usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine kwa kuandaa mwongozo wa malipo.

- Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya wahasibu na wakaguzi (NBAA), Bodi ya kusimamia manunuzi ya serikali (PPRA), pamoja na chuo kikuu Mzumbe imefanya mafunzo yafuatayo kwa wakuu wa idara pamoja na watumishi wengine:-

- Mafunzo /ufafanuzi wa sheria na kanuni za fedha za manunuzi za mwaka 2001.

- Mafunzo ya namna ya kutambua na kukabiliana na maeneo yenye vihatarishi vya kufikia malengo (risk areas).Mafunzo haya yameiwezesha wizara kuorodhesha maeneo hatarishi katika daftari "Risk Management Register" na kuweka mikakati ya namna ya kukabiliana nayo.

- Wizara imeweka na kuboresha mifumo mbalimbali ya udhibiti "Internal Control Systems" ambayo imeiwezesha kusimamia vizuri rasilimali za serikali na kupunguza hoja za ukaguzi kwa zaidi ya asilimia 50% kutoka hoja 60 kwa mwaka 2004/05 kufikia hoja 23 kwa mwaka 2007/08.

- Wizara kutokana na ushauri uliotolewa na wakaguzi imeweza kubadilisha mfumo wa kupeleka fedha za utekelezaji wa shughuli zinazofanyika mikoani kwa kuzipa ofisi zilizo chini ya wizara zilizoko mikoani, jukumu la kupokea na kusimamia fedha kwa kushirikiana na ofisi za hazina ndogo au wahazini wa halmashauri. Hatua hii imesaidia mtiririko wa taarifa za fedha, kazi zilizofanyika na kumbukumbu za serikali kurahisisha ukaguzi wa tathmini ya kazi husika.

  Aidha hatua hiyo pia imeongeza usalama wa fedha za serikali kwa kuwa hakuna mtumishi anayepewa na kutembea na fedha nyingi taslim kwa sasa.

- Kutokana na ushauri wa wakaguzi wizara imeandaa orodha ya vifaa/mali za serikali "Master Inventory Register" pamoja na daftari la vifaa vya kudumu kwa muda mrefu. "Fixed Asset Register"

2.11 UGAVI

Majukumu ya kitengo cha ununuzi na ugavi ni kusimamia kazi zote za ununuzi wa vifaa, huduma na ushauri, utunzaji, ufuatiliaji, upokeaji na usambazaji vifaa. Pia kutunza kumbukumbu ya vifaa vizima na chakavu

Mafanikio

- Kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka, ambao umewasilishwa na kuidhinishwa na mamlaka ya kudhibiti ununuzi (PPRA) na wahisani wa mfuko wa pamoja (Basket Fund).

- Baada ya Serikali kuidhinisha, Wizara imeweza kuanzisha kitengo cha Ununuzi na Ugavi kinachojitegemea.

- Uwezo wa kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya ununuzi kwenye miradi mbalimbali umeimarishwa ambayo inagharimiwa na fedha za Serikali au wafadhili ukiwemo mfuko wa pamoja (Basket Fund). Hii pia inajumuisha shughuli zinazofanywa na taasisi zifuatazo; MNH, MOI, TFNC, TFDA, Ocean Road Hospital, KCMC, Bugando, MSD, na Halmashauri na Mikoa.

- Kuandaa, kusambaza na kuanza kutumia waraka wa kukasimu majukumu ya PMU na Bodi ya zabuni ya wizara (Delegation and Contract Out) kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Taasisi mbalimbali ambazo zinajitegemea, kuanzia Januari, 2008.

- Kujenga uwezo wa kuratibu taarifa mbalimbali za Wakaguzi wa Ununuzi (Procurement Auditor - AMPROC), Wakaguzi wa mtandao wa Bohari Kuu ya Madawa (PKF Consultant) ujulikanao kama ORION na taarifa za Mhakikimali Mkuu wa Serikali katika vyuo vyote, Hospitali za rufaa ambazo zipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

- Kujibu ndani ya wakati hoja za wakaguzi mbalimbali zitolewazo na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Procurement Auditor (AMPROC), Financial Auditor (PWC), Mhakikimali Mkuu wa Serikali, Wakaguzi kutoka PPRA na Wakaguzi kutoka World Bank/Basket Fund. n.k

- Kuboresha daftari la vifaa vya kudumu (Fixed Asset Register) vya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 baadhi ya mapungufu yamerekebishwa na kutolewa taarifa kwa wakati.

- Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia – Tanzania Country Office umeandaliwa mpango wa kuboresha kitengo cha PMU (Strengthening of PMU Action Plan). Mpango huo umekamilika.

2.12 MAWASILIANO

Kitengo cha mawasiliano ni kiungo kati ya Wizara na vyombo vya habari pamoja na wananchi katika kufafanua mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara.

Mafanikio

- Kuwepo kwa Msemaji wa Wizara kumerahisisha upatikanaji wa habari kwa haraka zaidi, kuliko ilivyokuwa awali ikitolewa na viongozi wa juu tu.
- Ufafanuzi na upatikanaji wa habari za Wizara kwa wananchi na wadau, umerahisishwa

- Kuwa na tovuti na kuweka habari mbalimbali za zinazohusu Wizara.
- Wizara imefafanua mambo mengi kwa wananchi kupitia mikutano na vyombo vya habari, kwa mfano ufafanuzi kuhusu matumizi ya vitendanishi na vifaa vya hospitali.

2.13 Hospitali Maalum

2.13.1 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili

Hospitali ya Taifa Muhimbili hutoa huduma za kibingwa za tiba, mafunzo na utafiti

Mafanikio

Ukarabati wa majengo yote ya kutolea huduma ya afya ikiwemo kuweka vifaa na samani mpya. ambao unatumia fedha za serikali na mkopo kutoka Benki ya Afrika (ADB). Katika kipindi cha mwaka 2005/2008 yafuatayo yamekamilika:

- Ukarabati wa maabara kuu,(Central Pathology Laboratory –CPL), vyumba vya upasuaji,wodi zote, huduma za Radiolojia na jengo la kuhifadhi maiti.

- Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), jengo la kisasa kwa ajili ya ushauri nasaha na matibabu umekamilika na yanatumika.

- Ujenzi wa uzio kuzunguka Hospitali umekamilika.

- Mashine ya MRI imenunuliwa na inatumika, ambapo imesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa waliokuwa wakilazimika kwenda nje ya nchi kufuata kipimo hicho.Jumla ya wagonjwa 122 wamepimwa tangu mashine ianze kufanya kazi tarehe 14 Desemba 2008.

- Uanzishwaji huduma za upasuaji mkubwa wa moyo.Wagonjwa 57 wamekwishafanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo kwa mafanikio makubwa.

- Kuboresha huduma za hospital kwa kutumia mfumo wa kompyuta, kuanzia huduma za wagonjwa, makusanyo ya mapato, huduma za maabara na ununuzi wa dawa na vifaa.

- Kuanza kutoa tiba ya macho kwa kutumia kifaa kiitwacho “laser” ambacho huwezesha kutoa tiba ya macho bila upasuaji wa kawaida.

2.13.2 Hospitali ya Rufaa ya Bugando

Hospitali ya rufaa ya Bugando inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, inahudumia wakazi wa mikoa 6 ya Kanda ya Ziwa, yaani Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Tabora na Shinyanga. Mikoa hiyo inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi milioni 13. Hospitali ina jumla ya vitanda 850.

Mafanikio:

- Hospitali ina uwezo wa kuzalisha dawa za sindano za “infusions” za aina mbalimbali na kutosheleza mahitaji ya hospitali. Aidha kiasi cha dawa hizo 56,390 zinazalishwa kwa mwaka.
- Hospitali inashirikiana na Chuo Kikuu cha Mt. Augustine, kufundisha madaktari na madktari 13 wamehitimu mwaka 2008 kwa mara ya kwanza. Vilevile inaendesha vyuo vitano vya Sayansi shiriki na Uuguzi. Hii inajumuisha madaktari wasaidizi, radiolojia, dawa na maabara.
- Upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti ambapo jumla ya maiti 53 zinahifadhiwa kutoka maiti 20 hapo awali.
- Kuanzisha huduma ya tiba kwa njia ya mtandao, unaowezesha madaktari bingwa kutoka nje ya nchi kutoa huduma hiyo.
- Kukamilika kwa chumba cha kisasa kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu(ICU)
- Ukarabati wa mabweni ya wanachuo, pamoja na ujenzi wa bweni la madaktari wanafunzi umekamilika.

2.13.3 Hospitali ya Rufaa ya KCMC

Hospitali ya rufaa ya KCMC inahudumia wagonjwa kutoka katika Kanda ya Kaskazini na huduma nyingine maalum kwa nchi nzima. Hospitali ya rufaa ya KCMC ina idadi ya vitanda 450.

Mafanikio

- Huduma za wagonjwa wa nje zimeboreshwa kwa kusogezwa karibu na idara husika kama vile huduma za mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo na figo (Urology), huduma za magonjwa ya ngozi, akina mama, watoto, na magonjwa ya pua, masikio na koo.

- Serikali imeweka mashine kubwa 2 za “X-ray” na “Ultra Sound” 1 , “C T Scan” 1 na “X-ray CARM” 1. Vifaa hivyo vinasaidia katika kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa na hivyo kutoa tiba sahihi;

- Hospitali iliweka televisheni kwenye kliniki zote kwa lengo la kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa, kuwapatia taarifa na kuelewa matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaburudisha. Vile vile spika zimefungwa kwenye wodi zote kwa ajili ya wagonjwa waliolazwa kupata elimu ya afya na taarifa mbalimbali zinazohusu huduma za afya;

- Hospitali imeanzisha kituo cha ushauri nasaha cha ANGAZA ili kuwapatia huduma za ushauri nasaha wananchi wa Moshi mjini kuhusu UKIMWI;

- Hospitali hutoa huduma bure za chakula kwa wagonjwa waliolazwa wodini;

- Hospitali inashirikiana na chuo kikuu cha Tumaini kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za afya katika hospitali.

- Kujenga jengo la huduma ya uchunguzi wa damu salama kwa msaada wa serikali na jengo la huduma ya wagonjwa wa nje (OPD). Ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika wodi ya wagonjwa mahututi, hospitali ilijenga

wodi ya pili ya wagonjwa mahututi (Intensive Care Unit). Aidha wodi zote ziliboreshwa kwa kufanyiwa ukarabati.

- Hospitali kwa kushirikiana na taasisi ya Elizabeth Glazier Foundation imekamilisha ujenzi wa kituo cha watoto wenye maambukizi ya UKIMWI.

2.13.4 Hospitali ya Rufaa ya Mbeya

Hospitali ya rufaa Mbeya inatoa huduma za kibingwa za tiba, ushauri, utafiti na mafunzo.

Mafanikio

- Ukarabati ufuatayo umekamilika; hospitali ya wazazi Meta, jengo la utawala, majengo 6 ya wodi, karakana, sehemu ya kuegesha magari na uzio wa hosteli ya madaktari waliopo mafunzo kazini (Intern Doctors).
- Mashine mbili za kisasa za X-ray na mashine moja ya ”Ultra Sound” zimenunuliwa na kutumika.
- Hospitali inafanya Utafiti wa chanjo ya UKIMWI.
- Kuanzisha huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa ambao mfumo wao wa figo umeharibika.
- Kuanza kutoa huduma ya upasuaji wa watoto wenye vichwa vilivyojaa maji.
- Ujenzi na ununuzi wa vifaa vya kitengo cha wagonjwa mahututi umekamilika.
- Ongezeko la wataalam(madaktari, wauguzi na wafamasia) wanaofanya mafunzo kwa vitendo kutoka 20 mpaka 45.

2.13.5 Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga

Mafanikio

- Kituo cha tiba na utengemano wa waathirika wa dawa za kulevya kimejengwa.
- Ukarabati wa mifumo ya maji safi na taka, na uwekaji uzio wa nje na ndani katika hospitali ya Mirembe umefanyika.Pia wodi, ofisi za utawala na kuta za ngome zimekarabatiwa.

2.13.6 Taasisi ya Saratani Ocean Road

Mafanikio

- Serikali imenunua vifaa vya kisasa vifuatavyo kwa ajili ya kutibu magonjwa ya saratani:
    - Mashine mbili za “Cobalt 60” zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5, Mashine mbili za “Intracavitary Unit” zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni mia mbili, “Simulator”, na “Treatment Plan Unit” vyenye thamani ya shilingi milioni 280 na Mashine mbili za “Gamma Cameras” ambazo zilizogharimu serikali jumla ya shilingi milioni 800;
- Mkakati wa Taifa wa kutoa huduma za saratani umekamilika na umeanza kutumika.
- Kwa wastani wagonjwa 2,500 kwa mwaka wenye aina mbalimbali za magonjwa ya saratani, hupata matibabu.
- Hospitali inatoa huduma ya Saratani ya Shingo ya mji wa uzazi kwa wagonjwa wa nje (OPD) ,wagonjwa wapya na wale wanaofuatilia matibabu ya saratani.
- Vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 800 vilipokelewa kutoka“International Atomic Energy Agency - IAEA” ambavyo vinasaidia kuboresha huduma za tiba ya mionzi,aidha Serikali imechangia shiling milion 900 kwa ajili ya huduma hii.

- Mradi wa kuboresha huduma za tiba ya mionzi (Improvement of Radiotherapy Services Project) ulianzishwa katika hospitali hii. Mradi huu umekuwa ukitekelezwa na serikali ya Tanzania kwa kuchangia shilingi milioni 900 pamoja na “International Atomic Energy Agency - IAEA” kwa kutoa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 800. Mradi huu unawasaidia sana wagonjwa wa saratani katika kiwango cha hali ya juu.

- Mafunzo ya kutoa matibabu ya Saratani yameanzishwa.

2.13.7 Hospitali ya Kibong’oto

Hospitali hiyo hutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya kifua kikuu. Wagonjwa wanaolazwa ni wale wanaoletwa kutoka hospitali za mikoa na wale wanaokuja kutibiwa bila rufaa.

Mafanikio:-

- Majengo yamekarabatiwa ili yawe na uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wa kifua kikuu sugu na kufuatilia mwenendo wa vimelea sugu wa kifua kikuu .
- Majokofu mapya mawili yenye uwezo wa kuhifadhi maiti sita katika chumba cha kuhifadhia maiti yalinunuliwa kwa gharama ya shilingi milioni 30.0. Aidha upanuzi wa chumba cha kuhifadhia maiti kwa kutumia fedha za uchangiaji umefanyika.

2.13.8 Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

Mafanikio:

- Taasisi imeanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani ya mifupa (Mmed. Orthopaedic na Traumatology) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Jamii Muhimbili.

- Huduma za fani ya mifupa, upasuaji wa ubongo na mifumo ya fahamu zimeboreshwa. Idadi ya wagonjwa waliopata huduma hizi kuanzia 2005 jumla ya wagonjwa 166 wamefanyiwa upasuaji wa kuweka nyonga bandia na 39 wamefanyiwa upasuaji wa kuwekewa goti bandia.

Mwaka	2006	2007	2008
Mahudhurio ya wagonjwa wa nje	26,425	32,128	37,471
Wagonjwa walio lazwa	4,342	5,237	5,297
Upasuaji	2,576	3,087	3,396
Upasuaji Maalum			
▪ Nyonga	22	79	82
▪ Goti	-	-	39
▪ Uti wa mgongo	-	97	31
▪ Ubongo	52	85	94
Mazoezi ya viungo	13,536	15,339	30,049
Viungo bandia	516	699	838

2.14 WAKALA

2.14.1 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

Mafanikio

- Kanuni, miongozo na taratibu za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zimeandaliwa na kuziboresha ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003.

- Mkataba wa Huduma kwa Wateja ulitayarishwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuweka viwango vya ubora wa utoaji huduma.
- Toleo la kwanza la kitabu cha taarifa za dawa (Tanzania National Formulary – TNF) imefanyiwa mapitio na kuongeza maelezo yanayoenda na wakati kwa watoa huduma ya afya na kitabu hiki kinatumika kama rejea kwa watoa dawa katika ngazi zote.

- Vipindi vya redio 28 na matangazo mafupi 17 ya redio, ikiwa ni pamoja na vipindi 6 vya televisheni na mchezo mmoja wa kuigiza wa televisheni vilirushwa katika vituo mbalimbali kwa lengo la kuelimisha umma juu ya ubora, usalama na matumizi sahihi ya dawa, vyakula vipodozi na vifaa tiba. Aidha , matamko 49 yanayohusu udhibiti wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.
- Katika kufuatilia ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, sampuli 1,546 zilichukuliwa kutoka sokoni na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ambapo sampuli 1,274 zilifaulu. Aidha, jumla ya kesi 33 zinazohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Chakula, Dawa, na Vipodozi ya mwaka 2003, zilifikishwa katika vyombo vya dola ikiwa ni pamoja na mahakama.

- Katika kuimarisha mapambano dhidi ya bidhaa za chakula, dawa na vipodozi bandia, TFDA kwa kushirikiana na jeshi la Polisi imeanzisha Kikosi kazi cha kupambana na bidhaa bandia. Aidha Opersheni maalumu ya kukamata dawa bandia ijulikanayo kama “Operesheni Mamba” ilifanyika katika kipindi hiki kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, INTERPOL, FCC, MSD, TRA na TBS.
- Mamlaka imekamilisha mradi wa ujenzi wa ofisi mpya za Makao Makuu na kuizindua rasmi tarehe 1 Julai 2008.Aidha, ofisi tatu za Kanda za TFDA zilifunguliwa katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya ili kuimarisha na kupeleka huduma za udhibiti karibu zaidi na wananchi.

- Mpango wa maduka ya Dawa Muhimu (DLDM) umetekelezwa kwa kushirikisha sekta binafsi na umma kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu na huduma bora za dawa katika maeneo ya vijijini na miji midogo. Hadi sasa mpango umeenezwa katika mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Mtwara na Rukwa.

2.14.2 Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

Mafanikio

- Kuwa na uwezo wa kufanya uchunguzi na kutoa matokeo kuhusu uhalali wa mtoto kwa mzazi wa kiume, watoto wanaozaliwa na jinsia mbili ili kutambua jinsia iliyo na nguvu , magonjwa ya kurithi, ubakaji, ujambazi na mauaji kwa kutumia mtambo wa vinasaba (DNA).

- Tanzania imepata zawadi ya mshindi wa kwanza katika miradi ya ubunifu katika Utumishi wa Umma Barani Afrika (All Africa Public Sector Innovation Award.) mwaka 2008 kwa usimamizi mzuri wa matumizi ya kemikali nchini.
- Maabara mbili za Mkemia mkuu zimeanzishwa katika kanda ya Ziwa jijini Mwanza na Kanda ya Kaskazini katika Manispaa ya Arusha. Lengo

nikuharakisha utoaji huduma bora na ushauri wa kitaalam kwa wakati na kupunguza gharama ya kufuata matokeo ya uchunguzi Makao Makuu.

- Kuwa na jengo jipya la maabara na ofisi lenye ghorofa nne kwa ajili ya shughuli za mkemia mkuu wa Serikali.
- Wakala imekuwa na uwezo wa kufanya uchunguzi kutokana na ununuzi wa mitambo ifuatayo:-
  - GC/MS kwa ajili ya uchunguzi wa dawa za kulevya na viuatilifu
  -UV/VIS-NIR kwa ajili ya uchunguzi wa dawa za asili na za kutengenezwa
  -3100 EA (Elemental analyser) kwa uchunguzi wa sulphur na Nitrogen kwenye mafuta
- Uhusiano wa kimataifa katika usimamizi wa kemikali umeimarishwa kupitia mradi wa `Strategic Approach om International Chemical Management (SAICM).

2.14.3 Bohari ya Dawa (MSD)

- Upatikanaji wa dawa katika hospitali na zahanati ambao umepanda katika kipindi cha miaka mitatu toka asilimia 55 hadi 90 nchi nzima.
- Kuboresha huduma za kanda zote kwa kuajiri wafanyakazi nane wa kushughulikia malalamiko ya wateja.
- Mfumo wa ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa ziendazo kwa wateja umeanzishwa kwa kushirikiana na TFDA.
- Kuanzishwa kwa mfumo ambao hospitali zinaagiza bidhaa kulingana na bajeti, hii imeondoa tatizo la madeni sugu kwa MSD.
- Wateja wakubwa 412 kati ya 500 wameelimishwa kuhusu taratibu mbalimbali za utoaji wa huduma za usambazaji dawa, hii imesaidia kushughulikia mahitaji ya wateja kwa wakati.
- Mfumo wa ugavi shirikishi umeanzishwa na unatumika katika mikoa 18 ya Tanzania Bara kwa ajili ya kuleta ufanisi kwa kupunguza urasimu katika uigizaji na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.
- Bohari ya kanda ya kati imefunguliwa katika mkoa wa Dodoma ambayo inatoa huduma katika mikoa ya Dodoma, Singida na Halmashauri za Kiteto na Kilosa.Pia ujenzi wa bohari mpya ya Moshi umekamilika na unatoa huduma ya kufunga dawa(Packaging) kwa ajili ya vituo vya afya na Zahanati katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha. Kadhalika Ujenzi wa bohari ya aina hii kwa kanda umekamilika.
- Kuongeza uwezo wa maghala hadi kufikia mita za mraba11,687 kutoka mita za mraba 3,615, pamoja na kuongeza magari ya kubebea dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka magari 21 hadi kufikia magari 45.

2.14.4 Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania

2.14.4.1 Kudhibiti upungufu wa madini joto

Tatizo la upungufu wa madini joto mwilini limeendelea kupungua kutokana na kuwajengea uwezo wazalishaji chumvi wakubwa na wadogo kuweza kuongeza madini joto kwenye chumvi wanayozalisha.

Mafanikio

- Wazalishaji chumvi wakubwa wanane na zaidi ya wazlishaji wadogo 5000 wamepatiwa kilo 5000 za madini joto, pampu 4650 za kunyunyizia madini joto kwenye chumvi na jumla ya chupa 93,750 za kemikali za kupimia uwepo wa madini joto kwenye chumvi (*Iodine test solution*).
- Maabara ndogo zimeanzishwa katika wilaya za Tanga, Bagamoyo, Kinondoni, Kilwa, LIndi na Mtwara ili kupima viwango vya madini joto iliyopo kwenye chumvi inayozalishwa katika maeneo hayo.
- Asilimia 83 ya kaya nchini zinatumia chumvi yenye madini joto na tatizo la uvimbe wa tezi la shingi limedhibitiwa. Hivi sasa ni asilimia saba (7) tu ya Watanzania wenye tatizo hilo.

2.14.4.2 Udhibiti wa upungufu wa vitamini A

- Matone ya vitamini A na dawa za minyoo zinatolewa mara mbili kila mwaka kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika wilaya zote za Tanzania Bara. Zaidi ya asilimia 90 ya watoto waliolengwa walipatiwa huduma hizi.
- Utoaji wa matone ya vitamini A unafanyika sanjari na uhamasishaji wa uzalishaji, hifadhi salama na ulaji wa vyakula vyenye vitamini A na madini kwa wingi katika jitihada za kukabiliana na tatizo la upungufu wa vitamini A nchini.

2.14.4.3 Kuboresha unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wadogo

- Watoa huduma 100 wamepata mafunzo kuhusu unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo yanayojumuisha ushauri nasaha kuhusu

unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

- Sheria ndogo inayosimamia uuzaji na usambazaji wa maziwa mbadala na vyakula vya watoto wachanga ya mwaka 1994 ilidurusiwa ili kuboresha usimamiaji wa uuzaji wa vyakula hivyo kuimarisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama na kuendeleza lishe ya watoto wachanga.
- Hospitali 68 zimefanikiwa kuwa Hospitali Rafiki za Mama na Mtoto zinazolenga kuboresha hali ya afya na lishe ya watoto nchini.

2.14.4.4 Lishe na UKIMWI

- Watoa huduma majumbani 111 katika wilaya 37 za mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Mbeya, Rukwa na Iringa wamepata mafunzo kuhusu lishe kwa wagonjwa wenye UKIMWI.
- Nakala 17,000 za mwongozo wa kitaifa kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI, zimechapishwa na kusambazwa kwenye hospitali, Vyuo vya Afya na Taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI.

- Utafiti wa chakula kinachofaa kuongeza virutubishi vya vitamini na madini kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI umefanyika. Tafiti hii imeonyesha Chakula hiki ambacho kinatokana na mazao yanayopatikana hapa nchini kimeonyesha uwezo wa kuboresha Afya ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI. Chakula hiki kinatokana na mchanganyiko wa unga wa mahindi, soya pamoja na virutubishi vya madini na vitamini ambavyo vyote vinapatikana humu humu nchini. Matokeo ya awali yameonyesha kuwa afya ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI waliotumia chakula hiki imeimarika.

2.14.4.5 Uenezaji wa Teknolojia ya usindikaji bora wa unga wa muhogo na vyakula vya watoto

- Wakulima 127 wa muhogo katika wilaya zinazolima kwa wingi zao la muhogo za Rufiji, Newala, Kigoma, Kibondo, Kasulu na Kibaha wamepata mafunzo ya uhifadhi, usindikaji na matumzi ya zao la muhogo. Mafunzo haya yalilenga kuongeza ubora wa zao la muhogo na unga wa muhogo.
- Wakufunzi 130 katika Halmashauri za Manispaa 12 za Tanga, Moshi, Arusha, Ilala, Kinondoni, Temeke, Mbeya, Iringa, Songea, Musoma, Ilemela na Nyamagana wamepata mafunzo yanayohusu ubora na usalama wa vyakula vya watoto na teknolojia asili za kuboresha vyakula hivyo.

2.14.4.6 Elimu ya Lishe kwa Wanahabari

- Wahariri 10 na waandishi wa habari 22 kutoka vyombo mbalimbali vya utangazaji vya Umma na binafsi wamepata mafunzo ya ukusanyaji na utoaji wa habari na taarifa za lishe ili kuchangia katika kueneza elimu ya lishe kwa jamii.

2.15. Taasisi ya Tafiti za Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

Mafanikio

- Taasisi imekamilisha ujenzi wa ofisi mpya ya makao makuu Dar es salaam ambapo pia kuna maabara mpya na ya kisasa ya kuratibu na kufundishia kuhusu viwango na ubora wa maabara nchini (Quality assurance and training Laboratory). Aidha ukarabati/Ujenzi ofisi na maabara za Mbeya, hospitali ya Mkoa wa Tanga, Bombo, hospitali ya wilaya ya Korogwe, na Kituo kipya cha utafiti wa dawa asilia cha Ngongongare,Arusha umekamilika.
- Utafiti wa chanjo dhidi ya malaria umefanyika katika mikoa ya Tanga,korogwe ambapo katika utafiti wa awali unaonyesha kuwa chanjo hii inaweza kukinga watoto dhidi ya malaria kwa asilimia 56.
- Mpango wa Miaka Mitano wa Taasisi wa Utafiti, (NIMR Strategic Plan 2008 – 2013) umekamilika.

2.16 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NIHF)

Mafanikio

- Idadi ya Watanzania wanaohudumiwa na Mfuko huu imeongezeka kutoka asilimia 3 Desemba, 2005 hadi kufikia asilimia 5.2 ya Watanzania wote ilipofika Desemba, 2008. Lengo ni kuwafikia asilimia 45 ya Watanzania wote ifikikapo mwaka 2015.

- Kitita cha mafao kimeboreshwa na kinachojumuisha ongezeko la dawa 110 katika orodha ya awali ya dawa 445 ya mwaka 2005 na kufikia aina 555 mwaka 2008, ambazo zinatibu magonjwa yote ukiacha yale yaliyo katika mpango wa Serikali.

- Huduma za vipimo na uchunguzi wa maabara zimeongezeka kutoka vipimo 54 mwaka 2005 hadi kufikia vipimo137 mwaka 2008.

- Huduma za mafao ya miwani ya kusomea kwa wanachama wachangiaji zilmeanza kutolewa kuanzia mwezi Februari 2006.

- Mafao ya matibabu kwa Wanachama wastaafu na huduma kwa makundi maalum wakiwemo watu wanye ulemavu zinatolewa.

- Maduka ya dawa muhimu vijijini yapatayo 122 yameweza kusajiliwa na Mfuko kati ya Desemba 2005 hadi Desemba 2008, maduka haya yaliyoanza kusajiliwa mwaka 2006 yamesaidia sana upatikanaji wa huduma ya dawa kwa wanachama wa Mfuko katika wilaya za mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mtwara na Rukwa.

- Katika kipindi cha 2005-2008 mikopo nafuu ya vifaa tiba na ukarabati yenye thamani ya Shilingi Milioni 701.3 za Kitanzania vimetolewa kwa watoa huduma ambao asilimia zaidi ya 60 wako maeneo ya vijijini. Vifaa tiba vilivyolewa vimesaidia wanachama na wanachi kutibiwa karibu na wanapoishi na kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.Mikoa iliyopata mikopo hiyo ni Dar es Salaam,Pwani,Lindi,Morogoro,Dodoma,Rukwa,Mwanza na Kagera.

- Mfuko umekarabati Kliniki ya Ocean Road ya Jijini Dar es salaam inayotoa huduma za mfano kwa wanachama na wananchi kwa ujumla jijini.

3.0 HITIMISHO

Kutokana na mikakati mbalimbali iliyopo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii.Katika kipindi cha miak mitatu huduma nyingi zimeboreshwa na mafanikio yamepatikana hivyo kupunguza maradhi na vifo vya jamii ya watanzania.